

**DIWANI** apoteza mke na watoto ajali ya gari

UKURASA 3

**SERIKALI** yaelekeza makazi ya watu yatumike kulaza watalii Kilimanjaro

UKURASA 5



UKURASA 19

**MATOKEO DRC:** Rais Tshisekedi ang'ara kwa 77%, jeshi lawazima wanaoandamana

**HAALAND KUREJEA JANUARI MWISHONI**

UKURASA 21


# Nipashe

Ijumaa Desemba 29, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581539

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper


## RIPOTI MAALUM

# Mabasi usiku yawapa tabasamu wadau wote



**MIEZI** mitatu ajali mbili, zote mchana; msongamano abiria stendi watoweka...*Endelea Uk. 4*

Mabasi yakiwa stendi kwa kuanza safari usiku. **PICHA: MTANDAO**

UKURASA WA 12

**IJUE HIFADHI YA MTO UGALLA... INA MIAKA MINNE, UTAJIRI KIBAO, WATALII WAKUU WAZAWA**

KUNAPOTAJWA hifadhi ya taifa, maana yake kuna vivutio mbalimbali vya kipekee kitaifa. Hapo ndiko panapobeba maana hata

UKURASA WA 18

**TAWA YATOA UFAFANUZI MAMBA KUPIGWA RISASI HIFADHINI**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) imetoa ufafanuzi wa madai yanayotolewa dhidi yake kuhusu kuwapo kwa

# Rais Samia: Vyuo vikuu utafiti usiishie kabatini, tunauhitaji

UKURASA 2

**Katibu Mkuu aagiza wazazi kukagua watoto sehemu za siri**

UKURASA 3

**MICHEZO** **SIMBA YASAJILI WINGA MCOLOMBIA** UK. 24 **KATUNI** UK. 6

## RAIS SAMIA AAGIZA...

# Vyuo vikuu achaneni na utafiti wa kabatini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan ametunukiwa shahada ya udaktari wa heshima na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) huku akirejesha msisitizo wake vyuo vikuu kuzama katika utafiti ambao ripoti zake zitakabidhiwa serikalini kufanyiwa kazi.

Sambamba na hilo, Mkuu wa Nchi ameanika wasifu wa umahiri wake katika eneo la utalii na soko lake, ni zao la msingi uliojengwa kwake na Rais wa Sita wa Zanzibar, Amani Abeid Karume.

Rais alianika hayo jana wakati wa mahafali ya 19 ya SUZA, visiwani Zanzibar ambako alitunukiwa shahada hiyo ya udaktari wa heshima. Ni ya pili kwake baada ya kutunukiwa shahada ya aina hiyo na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) Novemba 30, mwaka jana.

Ni tukio la aina yake lililowakusanya Rais wa sasa na wa zamani, huku mwenyeji mkuu akiwa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, ambaye mzizi wake naye ni mwanazuoni wa chuo kikuu.

Katika ufafanuzi wake, Rais Dk. Samia alitaja maeneo makuu matatu ambako ripoti za utafiti wa kisomi zinahitajika sana kwa sasa, akiorodhesha: matumizi ya kiutawala serikalini, jamii na utaalamu wa uchumi wa bluu.

Alikosoa mwenendo wa kitaaluma uliopo ambao utafiti mwingi unaofanywa na wasomi, huishia kabatini baada ya kuhitimu, badala yake ripoti za utafiti huo ziwasilishwe kwenye mahitaji ili ziwe na manufaa endelevu.

Kwa mujibu wa Dk. Samia, mahitaji ya utafiti yako juu maradufu hivi sasa kuliko dunia ilikotoka, akisema "dunia ya sasa kila kitu ni utafiti".

**SABABU ZA KUTUNUKIWA**

SUZA imemtunuku udaktari huo wa heshima Rais Samia kutokana na mchango wake wa kuinua uchumi wa nchi kupitia sekta ya utalii. Mahafali hayo ya 19 ya chuo hicho yalifanyika Tunguu chuoni huko, nje ya Mji wa Zanzibar.

Baada ya kutunukiwa, Rais Dk. Samia alishukuru kutunukiwa shahada hiyo katika usimamizi wa utalii na masoko.

"Baada ya kupokea barua ya pendekezo la kunitunuku shahada hii, nikasema ngoja nijikumbushe nilichokifanya Zanzibar. Hivi nilifanyaje nikawatafuti nilifanya kazi nao? Wakaniambia kuwa nilifanya kazi kubwa ya kuimarisha utalii kabla sijawa Rais na baada ya kuwa Rais. Nikakumbuka ni jambo la kweli," alisema.

Mkuu wa Nchi alisema hatua nyingine aliyokumbushwa kuwa ameifanya ni kuzunguka kwenye maabara mbalimbali duniani kuitangaza Zanzibar kama ni kituo kizuri cha utalii, kipindi hicho akiwa Waziri wa Utalii Zanzibar chini ya uongozi wa Rais Dk. Amani Karume.

Alisema alishiriki kufanya mchakato wa kuifanyia marekebisho Bustani ya Forodhani na kusimamia vizuri sekta ya utalii kwenye kipindi kigumu kiuchumi mwaka 2008 na wakati huo kulizuka homa ya mafua.

"Tulijitahidi kudhibiti taarifa za magonjwa yale yasitoke ili watalii waendelee kuja nchini na tulifanya vyema watalii walikuja. Tulieleza mikakati tuliyoibuni ya kufungua sekta ya utalii na kuitangaza nchi na vivutio vya utalii kupitia filamu ya (Tanzania The ) Royal Tour," alisema.

Rais Samia alisema mbali na filamu hiyo, amefanya filamu nyingine na mwigizaji wa Kichina na filamu hiyo, karibu itatoka na itawavutia watalii wengi kutoka China ambapo filamu hiyo inaitwa "Kijiji cha Milele".

Alisema kuwa wakati anafanya yote hayo, dhamira ilisukumwa kwa kuwaletea maendeleo wananchi na kuimarisha ustawi wao na wala hakuwaza kwamba ipo siku jitihada hizo zitaonekana na kutunukiwa heshima kubwa kama hiyo aliyotunukiwa na SUZA. "Wanasema ukiona vimeelea vimeundwa. Sasa ninapopokea heshima hii ninapokea kwa watanzania wote wanaoendelea kunipa moyo na ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu," alisema.



Rais Samia Suluhu Hassan na viongozi wengine akiwa kwenye maandamano ya Kitaaluma wakati walipokuwa wakiingia kwenye ukumbi wa Dk. Ali Mohamed Shein Kampasi ya Tunguu kwa ajili ya kushiriki Hafla ya Mahafali ya 19 ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) jana, ambapo chuo hicho kimemtunuku Shahada ya Heshima ya Uzamivu kwa kutambua mchango wake wa kuifungua nchi kiuchumi kupitia Sekta ya Utalii. **PICHA: IKULU**

Alimshukuru Rais mstaafu, Amani Abeid Karume kwa malezi na miongozo na kumpa nyadhifa kubwa za uongozi serikalini ikiwamo uwaziri.

Akitaja sababu za kumtunuku Rais Samia kutunukiwa shahada hiyo, Makamu Mkuu wa chuo hicho (Taaluma), Dk. Ali Makame Ussi, alisema kuwa Rais Samia ameimarisha sekta ya utalii kupitia filamu yake ya Tanzania The Royal Tour, ambayo imezaa ongezeko kubwa la watalii na kuongezeka kwa wawekezaji.

Rais Samia pia aliwataka wahitimu wa chuo hicho kubadilika na kuwa na mawazo chanya kwa kuwa kuna changamoto za maisha, hivyo ni vyema kuzikabili.

Alisema amefarijika baada ya kuona asilimia 58 ya wahitimu wa chuo hicho ni wanawake. Ni matokeo makubwa ya jitihada zilizofanywa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ).

"Wakati wetu sisi kila tukienda juu kielimu, idadi ya wanawake inapungua. Leo (jana) wahitimu wanawake ni asilimia 58, ni kazi kubwa iliyofanywa na serikali," alipongeza.

Akizungumzia sekta ya elimu, Rais Dk. Samia alisema serikali imeongeza bajeti ya Wizara ya Elimu na kukuza miundombinu ya elimu na hali ya maisha ya nchi itategemea ilivyofaulu katika kukuza na kutumia ujuzi na maarifa na kuendeleza afya za watu wake.

Alisema kwa mnasaba huo, serikali imekamilisha mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo huku mitaala ikifanyiwa marekebisho iendane na uhalisia huo. Kazi hiyo imefanywa kwa ushirikiano wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alihimiza vyuo kufanya utafiti wenye tija na wenye kuangazia vipaumbele vya maendeleo ya serikali na kutatua changamoto za kijamii na kuendeleza mifumo ya kidijitali.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na SUZA kukabiliana na changamoto zinazokabiliana nazo ambazo ni upungufu wa watalamu pamoja na kuwa na miundombinu bora.

Pia alipongeza wahitimu wanawake ambao ni asilimia 58, akiwataka watumie mafanikio yao kuleta mabadiliko chanya katika nchi na kutoa mchango mkubwa wa maendeleo.

"Kuhitimu isiwe mwisho wa masomo, ninatoa wito kwa wanafunzi wote pamoja na wanawake waliohitimu kujiendeleza zaidi na kuwa wabunifu katika nyanja mbalimbali," aliagiza.

Alitoa rai kwa SUZA kuendeleza ushirikiano na taasisi binafsi katika kuendeleza chuo na kutatua changamoto zinazokabili chuo hicho.

Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Muhammed Makame Haji, alisema chuo kimekuwa kinapata mafaniko makubwa mwaka hadi mwaka. Kupitia mradi wa Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Kiuchumi ya Afrika (BADEA), wamewezesha SUZA kujenga majengo 39 ya ghorofa ambayo yatakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 20,000.

"Benki hizi zimewezesha kutanua chuo na kuimarisha miundombinu mingineyo ya chuo na tunampongeza Rais Mwinyi na Mama Samia kwa kuunga mkono maendeleo ya chuo," alisema.

Katika mahafali hayo ambayo yalikuwa na wahitimu 2,102 kwa ngazi ya cheti hadi uzamivu wa fani mbalimbali, SUZA pia ilitoa tuzo kwa waliobuni uanzishwaji wa chuo hicho ikiwamo marais wastaafu Dk. Salmin Amour, Amani Abeid Karume na viongozi wengine waandamizi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NA 28213 YA MWAKA 2023**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA**
**MOSES PINIEL MNANGASHWA ................MAREHEMU**
**IMELDA LUDOVICK CHUWA....................... MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jaladakama wanaona inafaa kabla ya kutolewa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa Muombaji aliyeomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 15 mwezi JANUARI , Mwaka 2024.

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 27 Mwezi DISEMBA Mwaka 202

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA

**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**JONATHAN MICHAEL MIHAMBO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA NOAH YENYE NAMBA YA USAJILI **T679 DFM** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH/TR /RB/780/2023**

**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**LAURENT ROBERT BUGUMBA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **TOYOTA IST** YENYE NAMBA YA USAJILI **T741 CLK** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH/TR /RB/696/2023**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 14 LA 2021**

**RAMADHANI MFAUME MSELEMU...............................MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**SHIA DEBT MANAGEMENT AND AUCTION MART LTD.............................................MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**SHIA DEBT MANAGAMENT AND AUCTION MART LTD**
**POPOTE ULIPO/MLIPO**
**RAMADHANI MFAUME MSELEMU** Amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni ( Mwananyamala. Shauri husika limepangwa kusikilizwa tarehe 11/1/2024.............saa tatu Asubuhi mbele ya Mh. J.W. SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 19 Mwezi 12/ 2023

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NA 16 YA MWAKA 2023**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA**
**DANIEL SALEHE..................................MAREHEMU**
**ZEFRIN DANIEL SALEHE..................... MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jaladakama wanaona inafaa kabla ya kutolewa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa Muombaji aliyeomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 27 mwezi DISEMBA , Mwaka 2023.

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 21 Mwezi NOVEMBA Mwaka 202

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA

HABARI KITAIFA

# Katibu Mkuu aagiza wazazi kukagua watoto sehemu za siri

**Na Sabato Kasika**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Abeida Rashid Abdallah, ameelekeza wazazi na walezi wa kike kukagua watoto wao sehemu za siri ili kujua kama hawajafanyiwa vitendo vya udhalilishaji wa kingono.

Alitoa maelekezo hayo katika mafunzo ya kuwajenga uwezo wana kikundi cha Banaty yaliyofanyika Michenzani, Unguja juzi na kuhimiza wazazi na walezi kuwa karibu na watoto wao.

"Wazazi na walezi wa kike hamna 'vibakio' (sehemu za siri za mwanamume), hivyo ni vyema kuwa karibu na watoto hasa wa kiume waliofikia umri wa balehe kwa kuwauliza maswali bila ya kuonea haya pamoja na kuwakagua sehemu za siri kama ziko salama," alisema.

Abeida alisema ripoti ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaonesha matukio ya udhalilishaji 199 yameripotiwa kwa mwezi wa Oktoba mwaka huu. Kati yake, asilimia 78.9 yalifanywa dhidi ya watoto na asilimia 16.2 kwa wanawake.

"Hivyo, ni vyema wazazi na walezi wanawake kila mara kuwa karibu na watoto wao. Sisi wanawake hatuna 'vibakio', ni lazima tuwe karibu na nao tuwahoji kama hakuna mtu aliyeguza sehemu za siri," alisema.

Katibu Mkuu huyo aliwataka wasiishie kuuliza maswali, bali wawakague ili kujua kama wako salama na wasisubiri watoto wao kuzoeshwa alichokiita "mchezo mchafu".

Alitoa wito kwa washiriki wa mafunzo hayo ya ujasiriamali kuyatumia ipasavyo kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inatoa fursa ya mikopo kwa ajili ya kuwawezesha kiuchumi ili waongeze kipato na kujikwamua kiuchumi.

"Ukweli ni kwamba, umaskini unachangia kuwapo vitendo vya udhalilishaji ndani ya jamii, hivyo mkatumie vyema mafunzo hayo ili kujiongezea kipato na kuepuka vitendo hivyo," aliagiza.

Mtaalamu wa Afya, Dk. Ummulkulthum Omar kutoka Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja, Zanzibar alisema anakutana na kesi za watoto wa umri tofauti walioingiliwa kinyume cha maumbile na watu wa karibu, wakiwamo wa miezi minane, akivitaja ni vitendo vinavyosikitisha.

Awali Mratibu wa Mafunzo hayo ambaye pia ni Mkurugenzi wa televisheni ya mtandaoni ya Raha, Raya Hamadi Mchele, alisema lengo ni kuwapa elimu kundi la Banaty, inayojumuisha masuala ya afya, kujitambua na ujasiriamali ili wajikwamue kiuchumi.

Alifafanua kuwa kikundi hicho kilianzishwa miaka minane iliyopita kwa lengo la kusaidiana katika shughuli mbalimbali za kijamii, ikiwamo harusi na misiba.

# Diwani apoteza mke, watoto ajali ya gari

**Na Julieth Mkireri, CHALINZE**

FAMILIA ya Diwani wa Kabuku Halmashauri ya Wilaya ya Handeni mkoani Tanga, Nurdin Semnangwa, imepoteza maisha katika ajali barabarani iliyotokea alfajiri jana.

Ajali hiyo imetokea eneo la Mbwewe, Chalinze Wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani na kupoteza watu watatu akiwamo mke na mtoto wa diwani huyo na msaidizi wa kazi.

Aidha, watu wengine wawili wamejeruhiwa baada ya gari walilokuwa wakisafiria kugonga gari lililokuwa limeegeshwa barabarani katika eneo la Mbwewe, Chalinze.

Taarifa iliyotolewa jana mjini Kibaha na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, ilisema ajali hiyo ilitokea Desemba 28 majira ya saa 11: 45 alfajiri.

Lutumo alisema gari lenye namba za usajili T. 395 DWE aina ya Alphard likiendeshwa na Mohamed Athuman (40) liligonga kwa nyuma gari lenye nambari za usajili T. 300 CLE/ T.399 AUP aina ya Faw lililoegeshwa pembezoni mwa barabara na kusababisha vifo vya watu hao.

"Watu watatu akiwamo mtoto mchanga wamefariki dunia baada ya gari lao kugonga gari jingine lililokuwa likiendeshwa na Alphonce Bosco (55) kwa nyuma na kusababisha vifo na majeruhi wawili," alisema.

Aliwataja waliofariki katika ajali hiyo kuwa ni Zakia Mohamed (36), Nadim Nurdin (miezi 8) na Goleth (23), wote wakazi wa Kabuku Tanga na majeruhi Mohamed Athuman (40) na Alice Sangule (08).

Alisema uchunguzi umebaini chanzo cha ajali ni dereva wa gari T.300 CLE/ T.399 AUP aina ya Faw kuegesha gari kando ya barabara pasipo kuweka alama ya tahadhari kwa watumiaji wengine wa barabara.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, akizungumza na Timu ya Wataalamu ya Usimamizi wa Mradi kutoka Ofisi ya Rais (Ikulu), watekelezaji wa ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme kutoka Wizara ya Nishati, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na wataalam wengine wanaohusika na mradi huo, jana mkoani Pwani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA–MWANZA

SHAURI NA 419 LA 2023

TUJIJENGE TANZANIA LIMITED..............................................MLETA MAOMBI

DHIDI YA

1. SISI AUCTION MART & GENERAL BROKERS
2. EVELINA CHRISTINA KUMALIJA
3. BENJAMIN MUNGO..............................................WAJIBU MAOMBI
4. LEAH MAKWABU

KWA: SISI AUCTION MART & GENERAL BROKERS, EVELINA CHRISTINA KUMALIJA na LEAH MAKWABU

Mnafahamishwa kwamba Mleta Maombi hapo juu amefungua Shauri /Ombi dhidi yenu katika Baraza la Ardhi na Nyumba Mkoa wa Mwanza, Ombi hili limepagwa kutajwa tarehe 10/01/2024 katika Chumba cha Baraza, Barabara ya Makongoro Jengo lililo Mkabala na Mahakama ya Mwanzo Mwanza mjini na Mahakama ya Wilaya Nyamagana, Tanzania.

Kwa hivyo mnatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo nyie wenyewe, wakili wenu au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria.

KAENI-Mkijua kwamba kushindwa kufika, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila nyie kuwepo.

Imetolewa nami kwa Amri na Chapa ya Baraza leo tarehe 04/12/2023.

PAULOS L.S LEKAMOI

MWENYEKITI

BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA

MWANZA

217770002





# Mabasi ya usiku yawapa tabasamu wadau wote

## -Miezi mitatu, ajali mbili, zote mchana
## -Msongamano abiria stendi watoweka

Na Jenifer Gilla

UREJESHAJI wa safari za usiku za mabasi ya mkoani umetajwa kupunguza ajali za barabarani kwa kiwango kikubwa, pia kuondoa msongamano wa abiria vituoni.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Ramadhani Ng'anzi alibainisha hayo katika mazungumzo na mwandishi wa habari hizi kuhusu mafanikio na changamoto baada ya mabasi kuruhusiwa kusafirisha abiria kwa saa 24.

Ng'anzi alisema tangu kuanza majaribio ya safari hizo za usiku mwezi Agosti, mwaka huu na kuruhusiwa rasmi mwezi Oktoba mwaka huu, ajali kubwa za mabasi zilizoripotiwa ni mbili; zote zilitokea mchana.

Utaratibu wa safari za mabasi saa 24, ulianza rasmi Oktoba Mosi, mwaka huu baada ya serikali kujiridhisha kiusalama, mwamko wa wananchi, huduma za mawasiliano na miundombinu ya usafirishaji.

Kamanda Ng'anzi alisema tangu utaratibu huo uanze hakujatokea ajali ya usiku na kwamba ajali ambazo zilikuwa zinatokea msimu wa sikukuu za mwishoni mwa mwaka, zimepungua kwa kiasi kikubwa.

"Kulitokea ajali kubwa mbili tu, moja ilikuwa Novemba 26, mwaka huu pale Manyoni ambapo treni iligongwa na basi na kulikuwa kumepambazuka na nyingine ilitokea kule Lindi baada ya basi kupata hitilafu za kiufundi," alisema.

Mafanikio mengine ya safari za usiku, kamanda huyo alitaja zimeondoa msongamano wa abiria katika vituo vya mabasi wanaosafiri kila siku kwenda mikoa mbalimbali, hali iliyokuwa inatumiwa na baadhi ya wakatisha tiketi kupandisha nauli.

Alisema katika kuhakikisha usalama wa wananchi barabarani unaongezeka, wameimarisha doria katika barabara kuu kwa kuongeza idadi ya askari.



Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Ramadhan Ng'anzi.

### KUTOKA LATRA

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA), Salum Pazzy, alisema wamedhibiti ajali hizo kwa kuweka masharti yakijumuisha madereva kuendesha mabasi kwa saa nane tu na kubadilishana na mwingine ili kuepuka ajili zinazotokana na uchovu.

Pazzy alifafanua zaidi kuhusu udhibiti huo, akibainisha kuwa sasa wameweka kitufe cha utambuzi katika kila basi ambacho dereva hutakiwa kukibonyesha anapoanza safari na baada ya saa nane anapomaliza muda wake, anayempokea naye hutakiwa kubonyeza.

"Anapobonyeza kile kitufe, sisi huku tunamsoma kupitia mifumo yetu, hivyo tunafahamu kuwa dereva fulani sasa hivi anaendesha gari fulani, akimaliza muda wake dereva anayempokea naye anatakiwa abonyeze. Kwahiyo, tunawadhibiti kwa namna hiyo," alisema.

"Safari za usiku pia zimepunguza ushindani wa madereva wa mabasi barabarani kukimbizana ili kufika haraka kuliko mwingine wakidhani ni kuwavutia abiria, jambo lililokuwa linasababisha ajali za mara kwa mara," alisema.

Pazzy alisema kwa sasa mchezo huo haufanyiki kwa sababu mabasi yapo ya kutosha kiasi cha abiria kuamua mwenyewe aondoke na basi gani na wakati gani.

Alisema utaratibu huo pia umepunguza uhitaji wa magari ya ziada katika kipindi cha msimu wa sikukuu. Kwa mwaka huu wametoa leseni za muda kwa mabasi binafsi 56 tu.

Kadhalika, Pazzy alisema utaratibu huo wa safari za usiku na mchana umedhibiti mabasi yanayosafirisha abiria kiholela bila kusajiliwa na LATRA na kuwatoza bei kubwa kwa kuwa kwa sasa mabasi yaliyokuwapo yanajitosheleza.

Meneja wa Kampuni ya Mabasi ya Tashrif, Shabani Shemweta, alishukuru serikali kwa kuidhinisha utaratibu huo, akiutaja umesaidia kupunguza adha ya usafiri katika msimu huu wa sikukuu.

Alisema utaratibu huo umekuwa na faida kwao kwa sababu umeongeza mapato yao kwa kufanya biashara usiku na mchana.

### ABIRIA

Mfanyabiashara wa nguo za watoto kutoka Moshi, mkoani Kilimanjaro, Irene Shayo, alisema utaratibu huo umewapunguzia gharama za malazi na kuokoa muda wanapokwenda kufungasha mzigo Dar es Salaam.

Alisema kuwa awali iliwalazimu kulipia gharama za kulala hotelini na kukaa siku nyingi jijini humo, tofauti na sasa ambapo wakishanunua mahitaji yao wanakwenda moja kwa moja stendi kupanda mabasi na kurudi mkoani.

"Sasa hivi ninapanda basi la usiku ninaingia Dar es Salaam asubuhi. Ninakwenda Kariakoo moja kwa moja ninafungasha mzigo wangu, jioni ninaelekea Shekilango, ninapanda basi za Moshi. Kwa kweli, ninaipongeza serikali kwa uamuzi huu," alisema Irene.

Mkazi wa Mbezi, Elizabeth Shayo, alisema anachopenda katika usafiri wa usiku ni kuwa, "hakuna msongamano na usumbufu katika vituo vya mabasi, safari huwa fupi kwangu, kwa sababu ninatumia muda mwingi kulala.

"Kwa sisi wenye watoto ule msongamano wa stendi ya mabasi ulikuwa unakera sana. Mwaka jana nilinusurika kupoteza mtoto, nikachanganyikiwa wakati ninamtafuta nikampa mtu pochi kumbe hata simfahamu nikapoteza kila kitu."

### AJALI 2023

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wiki mbili zilizopita, kwa kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka huu, ajali zilizotokea ni 1,641. Kati yake, 1,057 zilisababisha vifo huku 451 zikisababisha majeruhi wakati ajali 135 zilisababisha uharibifu wa vyombo vya moto.

Ajali hizo zilisababisha vifo kwa watu 1,550. Kati yake, vifo vya wanaume vilikuwa 1,189, na wanawake 361.

Majeruhi katika kipindi hicho, walikuwa 2,562 na kati ya hao, wanaume walikuwa 1,721 na wanawake ni 841.

## HABARI KITAIFA

# Makonda: Viongozi wa dini dumisheni ushirikiano

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, amewaomba viongozi wa dini kuendelea kudumisha ushirikiano kwa viongozi wa chama na serikali kwa kutoa ushauri na miongozo itakayosaidia kuchochea maendeleo nchini.

Makonda aliyasema hayo jana alipokwenda kumsalimia Askofu wa Kanisa katoliki Jimbo la Geita, Dk. Flavian Kassala ofisini kwake ikiwa ni mwendelezo wa utaratibu wake wa kwenda kuwaomba ushirikiano, ushauri na miongozo mbalimbali viongozi wa kiroho wa madhehebu ya dini nchini na makundi mengine ya kijamii, utakaomsaidia katika utekelezaji wa majukumu yake.

Alisema anawashukuru viongozi wote wa dini nchini kwa ushirikiano wanaoendelea kuutoa na ameahidi watakuwa pamoja kuhakikisha nchi inakua kiuchumi na maendeleo kwa wananchi.

Vile vile, alisema viongozi wa dini ni watu muhimu na wapo tayari kupokea ushauri utakaotolewa na kuufanyia kazi kwa maslahi ya nchi.

"Ninawaomba viongozi wote wa dini nchini kudumisha ushirikiano kwa viongozi wa chama na serikali kwa kushauri na kutoa miongozo itakayowasaidia kuendelea kuwatumikia Watanzania kwa haki na ufanisi ili kugusa matumaini yao kwenye nyanja mbalimbali za maendeleo nchini," alisema Makonda.

Naye Askofu Kassala, alimtakia Makonda kila la kheri katika majukumu yake na kumuahidi viongozi wa dini wataendelea kutoa ushirikiano wao kuiombea nchi.

Alisema wataendelea kuwashauri viongozi na kuwapatia miongozo mbalimbali itakayowasaidia kuendelea kuwa watumishi bora kwa wananchi wanapotekeleza majukumu yao ya kuiongoza nchi kwa haki na upendo ili kudumisha umoja na mshikamano kwa Watanzania.

"Utumishi unaoufanya ni wa jamii, imani yetu tunapokubariki wewe tunabariki jamii yote ambayo unakwenda kuitumikia uendelee kujitoa na uwe baraka kwao hasa unapopokea magumu na changamoto za kiulimwengu," alisema Askofu Kassala.

Viongozi hao kwa pamoja wamefanya maombi ya kuliombea taifa na Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ni Mwenyekiti wa CCM, kuendelea kuwa na afya njema na kuwatumikia Watanzania.



Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi, Paul Makonda, akiwa na watawa pamoja Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Geita, Dk. Flavian Kassala, alipowatembelea jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

ONGEZEKO LA WAGENI

# Nyumba za wenyeji kutumika kulaza watalii

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SERIKALI imezindua mpango mahususi unaohusu matumizi ya nyumba za wenyeji zilizo na nafasi katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Kilimanjaro kwa ajili ya kukabiliana na idadi kubwa ya wageni wanaofurika kutoka nje ya nchi na nje ya mkoa huo.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki, alibainisha mpango huo jana katika Mji wa Moshi, alipokwenda kufunga Tamasha la KCF.

Alisema wizara hiyo imeshaanza kutengeneza mwongozo wa matumizi ya nyumba hizo ili kuendana na mahitaji ya watalii.

Mpango huo ambao umebuniwa na Taasisi ya Utamaduni wa Kilimanjaro (KCF), unaonesha kuwa wenyeji kunufaika na mpango huo uliopewa jina la 'Home Stay' kwa kupata mgawo wa asilimia 60, watoa huduma watapata asilimia 25 na asilimia 15 itakuwa gharama za uendeshaji za KCF.

"Watu wa Kilimanjaro tujipange kwa ajili ya Home Stay. Ni fursa pana ya kukuza uchumi wetu. Hata sisi wizara tumeshaanza kutengeneza mpango huu ambao tunaona una tija katika uchumi na sekta yetu ya utalii," alisema waziri huyo.

Waziri Angellah pia alikabidhi zawadi kwa vikundi vya washindi wa ngoma za asili na vijana waliofanya vizuri kwenye shindano la kuzungumzia vivutio vya asili katika maeneo yao kwa lugha fasaha za asili za makabila yao.

Awali Mwenyekiti wa KCF, Ansi Mmasi, alisema programu hiyo inatoa fursa kwa wananchi wa Kilimanjaro kujisajili na kuruhusu nyumba zao zitumike kwa malazi ya wageni watakaofika kwa shughuli mbalimbali za utalii na kutembelea vivutio vilivyomo mkoani mwao.

Katika tamasha hilo lililoanza Desemba 27 na kufungwa Desemba 28 mwaka huu, Watanzania mbalimbali waliojitokeza, walitembelea mapango ya asili ya Chaga Curve yaliyoko Marangu na Kibosho Kirima.

Kwa mujibu wa Mmasi, mkoa huo kuwa na vivutio vingi na si rahisi kwa siku moja kuvifikia vyote, na hivyo mpango huo ni sehemu ya kufungua njia kwa wakazi wa Kilimanjaro na Watanzania na wageni kutembelea vivutio mbalimbali vikiwamo vya asili vilivyopo maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Kilimanjaro.


Ujamaa Community Resource Team
EMPOWERMENT JUSTICE STEWARDSHIP
PO Box 15111, Arusha, Tanzania
www.ujamaa-crt.org

217770502

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI.

SHIRIKA LA UJAMAA COMMUNITY RESOURCE TEAM NI SHIRIKA LISILO LA KISERIKALI LINALOJISHUGHULISHA NA KUJENGA UWEZO WA JAMII KATIKA MASUALA YA UTAWALA BORA, ARDHI NA MAZINGIRA KATIKA MIKOA YA ARUSHA NA MANYARA.

SHIRIKA LINAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA LITATEKELEZA MRADI MPYA KAMA INAVYOAINISHWA HAPA CHINI KUANZIA JANUARI 2024 MPAKA DESEMBA MWAKA 2025

UCRT KWA UFADHILI WA RIGHT AND RESOURCE GROUP(RRI) ITATEKELEZA MRADI UJULIKANAO KAMA" STRENGTHENED PASTORALISTS LIVELIHOODS RESILIENCE AND LANDSCAPE GOVERNANCE IN NORTHERN TANZANIA " KATIKA WILAYA YA HANANG` KATIKA VIJIJI VYA MURERU, DIRMA NA MING`ENYI NA WILAYA YA NGORONGORO KATIKA KATA YA OLOLOSOKWAN, SOITSAMBU NA ARASH UTAKAOGHARIMU KIASI JUMLA YA SHILINGI ZA KITANZANIA 576,284,820

***MRADI HUU UITATEKELEZWA KWA KUSHIRIKIANA NA HALMASHAURI HUSIKA PAMOJA NA VIJIJI.***

**KWA MAWASILIANO ZAIDI director@ujamaa-crt.or.tz na manager@ujamaa-crt.or.tz.**

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tujifunze, tuige ya Milind Soman kutunza afya zetu

**DUNIA** ya sasa ina maradhi mengi na hasa yasiyoambukiza kama kisukari, figo, uzito kupindukia, saratani na moyo, ambayo pamoja na kuyatibu kitaalamu, michezo inaweza kuwa dawa isiyo na gharama.

Kanuni hiyo ya umuhimu wa michezo inadhihirishwa wiki hii na mwanariadha nguli wa India Milind Samon, aliyeko nchini kushirikiana na wadau kuhamasisha umuhimu wa michezo kulinda afya na utimamu wa mwili ambao ni tiba hasa zama hizi za maisha ya kubweteka.

Samon, anashirikiana na Shirikisho la Riadha la Tanzania, tasnia ya habari (media) , wanamichezo , waigizaji na wananchi kuonyesha kwa vitendo 'tiba michezo' ni dawa ya kutibu magonjwa mengi.

Kuanzia kesho atatembea na kukimbia kilometa 130 kutoka Dar es Salaam hadi Bagamoyo, wakati wa kuhitimisha mwaka 2023.

Akiwa Dar es Salaam kwa juhudi za Kidiplomasia za Ubalozi wa India, Somon, anasisitiza kuwa michezo hasa kutembea na kuacha kukaa sehemu moja ni tiba inayoondoa magonjwa, inayoimarisha afya ya mwili na akili lakini pia ikiwaleta watu wengi pamoja kwenye riadha hiyo.

Riadha anayoizungumzia ni 'Ultra Marathon' au kukimbia na kutembea umbali mrefu zaidi ambao umebadilisha maisha ya wenye afya na wagonjwa India.

Kwetu tunaona ni wakati wa Tanzania kuiga jambo jema la kujitibu na kuishi maisha ya kiafya bila gharama.

Tujue ni wakati wa kubadilika na kujifunza kutoka kwa mwanariadha huyu nguli ambaye anasema kukimbia kidogo kidogo na kutembea ni dawa ya kutibu maradhi mengi yanayowakabili wengi.

Anatuambia michezo hiyo haijalishi umri, maumbile, hali ya afya wala haina gharama.

Tunajua kuwa Watanzania wengi hasa wanaoishi mijini wamebweteka hawapendi kutembea, wanaogopa vumbi, jua kali, kuchafuka na 'kujitesa' lakini wakijitahidi kula na kuwa na uzito mkubwa ambao umewaletea maradhi.

Tunaamini kuwa kuona ni kuamini, kupitia vyombo vya habari tunapomuona Soman , tujifunze kwake tubadilike,tufanye mazoezi ya kukimbia na kutembea umbali mrefu kuondoa taka mwili.

Hizo ni pamoja na mafuta, lehemu au kolesto ambavyo ni vibonge vya mafuta yanayoganda ndani ya mishipa ya damu, tupunguze uzito usio na sababu na pia tuondoe sonona kwa kuchangamsha akili na kujipa nguvu mpya.

Tukisikiliza maelezo yake, anatumbia kuwa mama yake ana miaka 87 lakini pia anashiriki marathoni ya kukimbia na kutembea , familia yake na jamii inayomzunguka imeungana na kufanya michezo hiyo na sasa ni sehemu ya maisha yao na wameona faida.

Ni vyema nasi tukauona umuhimu wa kuachana na bodaboda na kutembea kila wakati na hata kukimbia kwa umbali mfupi kila mara.

Aidha, tupende kuitumikisha miili yetu badala ya kupumzika zaidi kupendelea kula na kunywa bila utaratibu, kukaa vijiweni, kuangalia televisheni na kunywa bia ili tuwe na utimamu.

Tunaomba serikali inapojenga miundombinu iangalie uwezekano wa kuweka barabara za michezo ambazo hazitaingiliwa na magari wala, bodaboda ili kuwapa wananchi hamasa ya kutumia huduma hizo kuboresha afya zao.

Kadhalika, tunashauri sehemu za kazi ziwe na huduma za michezo mfano viwanja na bafu ili kucheza,kuoga na kubadili nguo baada ya mazoezi kuwezekana. Ni vyema pia ujumbe unaoenezwa na Soman wakuufanya mwili uwe timamu ufundishwe kwa watoto wetu shuleni na vyuoni mijini na vijijini ili wafurahie kutunza afya kwa kufanya mazoezi , kushiriki michezo hasa kutembea na kukimbia mbio fupi ili kulinda na kuimarisha kinga ya mwili.

Tubadilike badala ya kuzoea magari na pikipiki na maisha ya kubweteka ambayo tunazioona athari zake ili tuwe na taifa lenye afya.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com







Muungwana Lazima Nilonge

Na Sabato Kasika

# Kwaheri 2023, ulikuwa mwaka wenye maambukizi ya Marburg

**MWAKA** 2023 ndio huo sasa unaelekea ukingoni, umekuwa ni mwaka wa safari ndefu yenye milima na mabonde, lakini furaha na huzuni katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Zikiwa zimebaki siku nne kabla ya mwaka 2020 kutia nanga, ninaona kuna haja ya kujikumbusha mambo kadhaa yaliyotikisa nchi hasa upande wa afya katika mwaka huu unaoelekea ukingoni.

Mwaka jana, nchi ilitikiswa na matukio makubwa, lakini ninataka nigusie upande wa afya, hasa ugonjwa usiojulikana, ambao ulivamia mkoani Kagera na kusababisha vifo vya baadhi ya wakazi mkoa huo.

Ugonjwa huo uliibuka Machi mwaka huu, katika vijiji viwili, wilayani Bukoba Vijijini mkoani Kagera, huku watu watano wakidaiwa kufariki dunia na kusababisha Wizara ya Afya kwenda kupiga kambi huko.

Wizara hiyo ililazimika kupiga kwa kushirikiana na wadau wengine wa afya, wakiwamo Shirika la Afya Duniani (WHO) na kuanza harakati na kukabiliana nao, huku ikichunguza chanzo chake.

Baadaye, serikali ilitangaza kuwa ni virusi viitwaavyo Marburg, ambavyo ni sawa na virusi hatari vya ebola, vilivyogunduliwa kwa mara ya kwanza baada ya watu 31 kuambukizwa, saba kati yao kufariki dunia mwaka 1967 huko Marburg na Frankfut, Ujerumani na Belgrade huko Serbia.

Ikaelezwa kuwa dalili za ugonjwa huo ni pamoja na kikohozi, maumivu ya viungo, kuhara na kutapika na mara nyingi hata upungufu wa damu katika mwili na kwamba virusi vya Marburg vilipatikana kwa mara ya kwanza kwa tumbili wa kijani kibichi wa Kiafrika.

Wizara ikafafanua kuwa mlipuko huo ulitokana na tumbili wa Kiafrika walioagizwa kutoka Uganda. Lakini pia virusi hivyo vimehusishwa na wanyama wengine tangu wakati huo.

Katika maelezo zaidi ikasema ugonjwa huo kwa binadamu, virusi vyake huenezwa zaidi na watu ambao wamekaa kwa muda mrefu katika mapango na migodi yenye popo.

Aidha, baadaye Juni mwaka huu, wizara ilitangaza rasmi kudhibitiwa kwa homa hatari ya virusi vya Marburg vilivyoripotiwa Machi mwaka huu na kugharimu maisha ya baadhi ya watu mkoani humo.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alitangazia dunia kuhusu kudhibitiwa na kumalizika kwa virusi vya homa ya Marburg, huku akishukuru jumuiya ya kimataifa hasa Umoja wa Ulaya.

Mbali na EU, akaiishukuru pia Marekani na Umoja wa Afrika (AU) kwa kutoa misaada mbalimbali iliyotumika katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo mpya ulioikumbuka Tanzania.

Wakati tunaingia mwaka mpya wa 2024, ninadhani hatuna budi kuchukua tahadhari zote zilizoelekezwa na wataalam wa afya kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa huo mpya uliodhibitiwa.

Ninaeleza hivyo, kwa sababu walieleza kuwa kudhibitiwa kwa ugonjwa huo haina maana kwamba hauwezi kurudi, bali unaweza kuibuka tena iwapo watu hawatafuata masharti ya kujinga nao.

Wanataja dalili za Marburg kuwa, homa, kuumwa vibaya na kichwa, kuumwa na misuli, na kwamba baada ya siku tatu dalili nyingine hujitokeza ikiwamo, kuhara, kuumwa na tumbo, kichefuchefu, kutapika.

Aidha, mwonekano wa wagonjwa katika awamu hiyo kwa macho ya ndani, nyuso zisizo na hisia na uchovu mwingi na kwamba baadhi ya watu hutokwa na damu sehemu mbalimbali za mwili na kufa siku nane hadi tisa baada ya kuugua kwa kupoteza damu nyingi na mshtuko.

Inaelezwa kuwa hadi sasa, hakuna chanjo iliyoidhinishwa ya ugonjwa wa Marburg, bali kuna chanjo mbalimbali ambazo zinaendelea kutengenezwa na WHO kwa kushirikiana na wadau wengine. Wakati chanjo ikiendelea kutafutwa, inashauriwa kujikinga na ugonjwa huo, kwa kuepuka kugusa majimaji ya mwili wa mtu mwenye dalili za Marburg kama damu, mate, matapishi, jasho, mkojo au na kinyesi.

Inashauriwa pia kutogusa au kuosha maiti ya mtu aliyefariki kutokana na ugonjwa wa Marburg bila kutumia vifaa kinga au kugusana na mtu mwingine kama kusalimiana kwa kupeana mikono kwa kukumbatiana.

Hivyo, mwaka 2024 uwe wa heri kwa kila mmoja wetu kuzingatia njia zote za kuepuka ugonjwa huo, ambazo zimeelekezwa na wataalamu wa afya, ikiwamo kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni.

HABARI KITAIFA

# Jamii yatakiwa kutembelea makao ya malezi ya watoto

**Na Raymond Mtani,** DODOMA

MENEJA wa Makao ya Taifa ya Kulelea Watoto Kikombo, jijini Dodoma, ameitaka jamii kutembelea watoto wanaolelewa katika makao ya kulelea watoto ili kuwajenga kisaikolojia kwa kuwa wengi wao wanatoka katika mazingira yenye historia ngumu.

Jonas Tarimo alitoa rai hiyo alipotoa taarifa kuhusu shughuli za makao hayo kwa wafanyakazi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) waliofika kutoa zawadi ya sikukuu mwishoni mwa wiki iliyopita.

"Watoto hawa wanatoka katika uzoefu mgumu, ndoa zenye migogoro, unyanyasaji na wengine hawana familia kabisa, hivyo mnapofika hivi wakaona sura mpya, mkaongea nao, mnatusaidia sana kuwajenga kisaikolojia," alisema Tarimo.

Meneja huyo alisisitiza kuwa msaada ni muhimu ingawa kufika katika vituo hivyo ni muhimu zaidi kwa kuwa ni watoto wa jamii, kuongea nao hupanua mawanda ya uelewa wao na kuwapa mtazamo mpya wa maisha.

Dk. George Dilunga, Bingwa wa Magonjwa ya Dharura na Mkuu wa Idara ya Magonjwa hayo BMH, anasema hatua ya kutembelea Makao ya Kitaifa Kikombo imetokana na uhusiano uliopo baina ya taasisi hizi mbili.

"Tumekuwa tukitoa huduma za afya kwa watoto wanaoishi hapa kwa kuwafanyia uchunguzi na matibabu kila baada ya miezi mitatu tangu Juni 16, 2021 yalipozinduliwa makao haya, hivyo wamekuwa sehemu ya familia yetu," alisema Dk. Dilunga.

Aliongeza kuwa uamuzi wa kujumuika nao msimu huu wa sikukuu, ulilenga kuongea na watoto hao kama sehemu ya kuwapa faraja msimu huu wa sikukuu.

BMH ilikabidhi nguo, vitambaa kwa ajili ya kushona sare za shule, seti maalum za mahitaji ya shule zilizohusisha madaftari, kalamu na rula kwa watoto zaidi ya 80 ambayo ni michango ya wafanyakazi wa Idara ya Magonjwa ya Dharura BMH.

Kuna zaidi ya watoto 24,000 wanaolelewa katika makao zaidi ya 320 yaliyosajiliwa katika sehemu mbalimbali nchini.

Watoto hao ni zao la migogoro ya ndoa, unyanyasaji, vifo vya wazazi, kutelekezwa na sababu zinginezo.



Mkuu wa Wilaya ya Hanang, mkoani Manyara, Janeth Mayanja (wa tatu kushoto), akipokea bati kutoka kwa Mwakilishi wa Kampuni ya Puma Energy Tanzania ambaye ni Meneja Uhusiano, Godluck Shirima (wa pili kulia). Wanaoshuhudia ni Meneja Masoko, Lilian Kanora (wa pili kushoto) na Meneja Rasilimali Watu Joseph Jaruma (kulia). Kushoto ni Ofisa Ugavi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang, mkoani Manyara Methew Giramisi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Wazazi/walezi waanze mwaka kwa kusimamia ulinzi wa mtoto'

**Na Sabato Kasika**

SHIRIKA la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI) limetoa salamu za mwaka mpya wa 2024, likiwataka wazazi, walezi na jamii kusimamia ulinzi na usalama wa watoto, ili kuwaepusha na ukatili wa kijinsia.

Mkurugenzi wa WAJIKI, Janeth Mawinza, alisema jana kuwa mwaka 2024 uwe wa kuwaleta pamoja wazazi na walezi kutafakari mustakabali wa watoto na kuwajenga kuwa viongozi bora, watendaji na wazazi bora wa baadaye.

"Uwe ni mwaka wa wazazi na walezi kutenga muda wa kuzungumza na watoto wao na kufahamu mienendo yao, marafiki na taaluma kwa ujumla na kudadisi changamoto zinazowakabili wawapo shuleni na nje ya shule, ili kuwaepusha na ukatili wa kijinsia na kujenga kizazi bora na salama chenye maadili mema," alisema Janeth.

Alisema kuwa kwa muda mrefu WAJIKI inatekeleza kampeni ya 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono kwa Wasichana na Wanafunzi Inawezekana', ikilenga kuliepusha kundi hilo na rushwa ya ngono.

"Katika kampeni hii tumekutana na mambo mengi ya kutisha ikiwamo baadhi ya wazazi kumalizana na wale wanaowafanyia watoto wao ukatili, lakini pia ukosefu wa elimu kuhusu ukatili wa kijinsia," alisema.

Alisema ulinzi wa watoto unaanzia kwa wazazi, wazazi kisha jamii na kwamba mwaka ujao ulinzi huo ungeongezeka zaidi ili kupunguza wingi wa matukio ya vitendo vya ukatili wa kijinsia ndani ya jamii.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya WAJIKI, Kalunde Mongomongo alisema kuwa awali shirika hilo lilianza kampeni ya kupinga rushwa ya ngono kwa wanafunzi kwa kushirikisha madereva wa bodaboda, bajaj na daladala na sasa linashirikisha makundi mengine.

"Tunafanya kazi katika wilaya za Kinondoni, Ilala na Temeke mkoani Dar es Salaam, tukifadhiliwa na Women Fund Tanzania (WFT), sasa tumeyafikia makundi ya jogging," alisema Kalunde.

Kutokana na kuendelea kuwapo vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia, Mongomongo alisema WAJIKI itaendelea kupambana navyo kwa kuwafikia waathirika wa vitendo hivyo na kutafuta suluhu ili kujenga jamii bora.

"Lakini tunaishukuru serikali kwa mikakati yake mbalimbali ya kutokomeza ukatili kwa watoto na wanawake kupitia sera na sheria zinazolinda haki za watoto dhidi ya vitendo vya ukatili," alisema.

Ofisa wa Idara ya Tathmini na Ufuatiliaji wa WAJIKI, Hans Obote, alisema ushirikiano kati ya serikali na wazazi kuanzia ngazi ya mtaa ni muhimu, hasa kufanyia kazi malalamiko yanayopelekwa husuan ya ukatili wa kijinsia na si kuyamaliza kifamilia.

"Ninaamini kila upande ukitambua wajibu wake, itakuwa rahisi kufanikisha kampeni yetu katika mwaka ujao, kwani sote tunatamani kuwa na kizazi bora cha baadaye," alisema Obote.

KABWELA Na Fadhili Mohammed



# RC Pwani awageukia viongozi wasiofuatilia wanafunzi watoro

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

SERIKALI mkoani Pwani imesema kiongozi wa serikali wa ngazi ya kijiji na kata ambaye hatafuatilia watoto ambao hawaendi shule kwa sababu mbalimbali atashughulikiwa kwa kuwekwa pembeni kutokana na kushindwa kuwajibika kwenye nafasi yake.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, ameyasema hayo jana alipokuwa akizungumza kwenye kikao cha wadau wa elimu kilichofanyika mjini hapa na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali.

"Nikifika sehemu kuna watoto hawasomi najua anatoka eneo fulani kiongozi wa eneo hilo nashughulika naye sio kazi ya mkuu wa mkoa, sio kazi ya mheshimiwa mkuu wa wilaya kwenda katika ngazi ya kijiji na kata eti anafuatilia wakati kiongozi wa ngazi ile yupo."

"Sasa kama kiongozi huyo anashindwa kutuambia kazi imenitosha anaona aibu yeye aache tu watoto wasiende shule tutamsaidia kumuweka pembeni, haiwezekani tuone kwenye mitandao watoto hawaendi shule, tuone kwenye mitandao mambo ya ovyo kabisa kuna sehemu watoto wanakaa chini, vyumba vya kusomea vipo vya ovyo, watoto wanasomea kwenye miti kiongozi upo pale haiwezekani, tunaanza na wewe," alisisitiza.

Alisema baadhi ya viongozi wanachagua mambo ya kufanya na hata wakikutana na vikwazo hawatoi taarifa ngazi za juu na kwamba ofisi yake itafanya ziara za kushtukiza kuona utekelezaji wa maagizo.

Kadhalika, alisema hakuna sababu ya serikali kuwa kikwazo kwa mwanafunzi kuanza masomo shule zikifunguliwa hata kama hajakamilisha suala la sare za shule.

Ofisa Elimu Mkoa wa Pwani, Sara Mlaki alisema mkoa huo unalenga kuandikisha wanafunzi wa darasa la kwanza 51,446 kwa mwaka 2024 na hadi kufikia Desemba, mwaka huu kuna wanafunzi 35,997.

Akizungumzia vikwazo kwa mkoa huo, alisema upo upungufu wa miundombinu ya shule ikiwamo madarasa, nyumba ya vyoo maabara, meza na viti pia, utoaji wa chakula bora chenye virutubisho pamoja na utoro wa rejareja bado ni kikwazo.

Aisha alibainisha wanafunzi 3,005 wa shule za msingi na sekondari waliokatisha masomo kwa utoro kwa sababu mbalimbali huku waliopata mimba wakitajwa kuwa ni 179, shule za msingi wakiwa ni 134 na sekondari 45. Mkoa wa Pwani umepata ufaulu wa asilimia 83.72 kitaifa na waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wakiwa ni 41,028 wasichana 21,552 na wavulana 19,476.



Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Prof. Elifas Bisanda (kulia), akifungua kikao kazi cha Kamati ya Uongozi wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Uchumi (HEET), Bagamoyo, mkoani Pwani jana. Wa pili kulia ni Naibu Makamu Mkuu wa Chuo -Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu, Prof. Deus Ngaruko ambaye ni Mratibu Mkuu wa Mradi wa HEET wa OUT. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Naibu Waziri ampa tano Kamanda Ng'anzi

**Na Sabato Kasika**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani, Jumanne Sagini, ameridhishwa na kazi inayofanywa na Kikosi cha Usalama Barabarani ya kutoa elimu kwa madereva wa mabasi na vyombo vingine vya moto, wakati huu wa kuelekea mwisho wa mwaka ili kuepusha ajali za barabarani. Alisema kwa njia hiyo watampunguzia Rais Samia Suluhu Hassan, majonzi ya kutuma salamu za pole kwa wakuu wa mikoa kutokana na ajali zinazosababisha vifo, majeruhi na ulemavu wa kudumu. Sagini alisema hayo katika salamu zake alizomtumia Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, SACP Ramadhan Ng'anzi, kumshukuru kwa jinsi anavyofanya kazi hiyo vizuri kwa kushirikiana na wadau wengine. "Hakika Kamanda Ng'azi na vijana wako mmetendea haki jukumu mlilopewa la usimamizi wa sheria za usalama barabarani. Binafsi nimeridhika jinsi timu ya trafiki na LATRA mlivyoshirikiana kusimamia utekelezaji wa sheria ya usalama barabarani kwa vitendo," alisema.

Alisema, ameona jinsi walivyoweka mkazo katika utoaji wa elimu na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria madereva wakaidi wa sheria ili kutoa fundisho kwao na kwa wengine ambao wangejaribu kuiga uvunjaji wa makusudi wa sheria za usalama barabarani.

"Nimefurahi pia kuona mkishirikisha kamati za usalama barabarani za mikoa na wadau wengine wa usalama barabarani. Ninaamini Tanzania bila ajali inawezekana, kila mmoja atimize wajibu wake," alisema Sagini.

Kamanda Ng'azi alisema operesheni inayoendelea sasa wakati huu wa kuelekea mwisho wa mwaka, haitawaacha salama madereva wa bajaj na bodaboda wanaovunja sheria ya usalama barabarani.

Alifafanua kuwa pamoja na kutoa elimu, wamekuwa wakipima kiwango cha ulevi kwa madereva wote kabla ya kuanza safari, ili wasisababishe ajali zinazotokana na kuzidiwa na pombe.

Ng'anzi alisema hayo mjini Morogoro juzi, wakati akikagua bajaj na bodaboda zilizokamatwa kwa makosa mbalimbali yakiwamo madereva wa bodaboda kupakia abiria zaidi mmoja na kutokuvaa kofia ngumu.

"Ninawalekeza madereva wa vyombo hivi kufuata sheria, taratibu na kanuni za barabarani ili kuepuka usumbufu wa kukamatwa kwa makosa ya kuvunja sheria ya usalama barabarani," alisema Kamanda Ng'anzi.

Aidha, Kamanda Ng'anzi aliwataka wakuu wa usalama barabarani wa mikoa yote kusimamia sheria hii madereva wa bodaboda wasibebe abiria zaidi ya mmoja, na kwamba wakionekana wakamatwe.

# Jamii yahimizwa kuwaheshimu, kuwathamini wazee

**Na Benny Kingson,** TABORA

KUTOKANA na madai ya wazee kuendelea kutotendewa haki kwenye huduma mbalimbali, jamii imehimizwa kurudi kwenye msingi wa maadili ya kuwaheshimu, kuwajali na kuwathamini kwa kuwapa kipaumbele.

Katibu wa Halmashauri Kuu NEC Oganazesheni wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Issa Gavu, alitoa wito huo alipokuwa akiongea na Baraza la Wazee wa chama hicho Mkoa wa Tabora kuwa wazee ni hazina ya chama na taifa ambao wanashauri kwa hekima, kurithisha yaliyo mema, kushauri na kuhifadhi malengo na madhumuni yaliyowekwa na wanapaswa kulindwa.

Gavu alihimiza makatibu wa CCM wa mikoani na wilayani kuitisha mabaraza ya wazee katika maeneo yao na kuhakikisha wanasimamia mabaraza hayo kila baada ya miezi sita na kuyaendesha kila wanapoona kunauhitaji ili kusikiliza kero zao na kuzitafutia ufumbuzi.

Aliwahimiza makatibu hao kuwasikiliza wazee na kuhakikisha kero zao zote zinazowakabili katika jamii wanazitolea taarifa na kuchukua hatua kwa kuzitatua zilizo ndani ya uwezo wao na kutambua kuwa ni haki yao ya msingi kupewa kipaumbele kupata huduma mbalimbali katika jamii.

Katika hatua nyingine amewaonya watu watakao wachezea madiwani na wenyeviti wa serikali wa maeneo husika kwamba watachukuliwa hatua za kinidhamu kwa kuwadharau viongozi waliochaguliwa kisheria na ni kosa kisheria.

Akizungumzia suala la rushwa alisema ni tatizo la jamii nzima hivyo linapaswa kuthibitiwa kwa vitendo na kwa dhati toka moyoni na pande zote mbili yaani mtoaji na mpokeaji kwa kukataa kutoa na kupokea na kuona ni janga na kuhakikisha kila mmoja anatimiza wajibu wake ili tija ipatikane kwa haki katika jamii.

Aliutaka Wakala wa Barabara Mijini na Vijini (TARURA) kusimamia matengenezo ya miundombinu ya barabara zote zilizopo katika maeneo yao na kumaliza changamoto zote sugu ambazo ni kero na kikwazo cha maendeleo ya jamii.

Mwenyekiti wa Wazee Kata ya Kanyenye, Manispaa ya Tabora, Remigius Kalugu (86), alisema kuwa umefika wakati mkoa huo kupewa hadhi na heshima inayostahili kutokana na viongozi wengi waliopita na waliopo madarakani kusoma na kufanya kazi mkoani humo.

"Tumepiga sana makelele na kulia kuhusu pale palipowekwa sanamu ya Mwalimu Nyerere kwamba patengenezwe vizuri majengo yake pafanane na hadhi ya mhusika," alisema.

Alisisitiza serikali na chama tawala kutendea haki wenyeviti wa serikali za maeneo kupata posho angalau za kujikimu maisha kwa kuwa wanafanyakazi kubwa na ngumu na kwamba wazee wote nchini wapatiwe mafao angalau kidogo bila kujali kama walikuwa watumishi wa umma.

Juma Dewji (80), mkazi wa Mwongozo Ulyankulu wilayani Kaliua akizungumzia suala la takrima alisema kuwa jina hilo limetumika vibaya kuhalalisha rushwa na imesababisha kushamiri na kutawala katika jamii na kuvunja demokrasia.

"Kuna haja ya somo la saikolojia kufundishwa shuleni na kuwekwa katika mitaala rasmi ili watoto wafundishwe kuwajengea uwezo na kudumisha maadili yao na uzalendo na hili zao la tumbaku nashauri liwe linakaushwa kwa umeme ili kuondokana na matumizi mabaya ya kuni yanayosababisha uharibifu wa mazingira na kuleta jangwa," alisema.





## Jumuiya za wazazi zatakiwa kujiimarisha kiuchumi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KATIBU Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Gilbert Kalima, amezitaka jumuiya za wazazi nchini kujiimarisha kiuchumi, kwa kuendeleza miradi waliyonayo katika maeneo yao pamoja na kuibua miradi mipya.

Aidha, ameiagiza mikoa ambayo haijaunda kamati ndogo kwa mujibu wa kanuni zanazoongoza jumuiya hiyo, kufanya hivyo mara moja ili zisadie kushughulikia masuala mbalimbali ya jumuiya hiyo ikiwamo uchumi.

Aliyasema hayo jijini Arusha wakati wa kikao maalum cha Baraza la Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Arusha.

Pia amewaagiza viongozi wa jumuiya hiyo katika mikoa yote nchini, kuhakikisha inaweka mikakati thabiti ya kusaidia CCM kushinda kwa kishindo katika uchaguzi wa serikali za mitaa, utakaofanyika mwakani pamoja na uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

"Hatuwezi kuwa na siasa safi katika jumuiya yetu kama hatutakuwa na uchumi imara, kwa sababu hii ninaziagiza jumuiya za wazazi katika mikoa yote hapa nchini, kuhakikisha wanaiendeleza miradi waliyonayo pamoja na kuibua miradi mipya," alisema.

Aidha aliupongeza mkoa wa Arusha kwa kuibua miradi mbalimbali ya uchumi pamoja na mradi wa maduka ambapo pia wanaendelea kuibua miradi mingi zaidi.

"Kipekee nampongeza sana Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Arusha, Hezron Mbise, kwa miradi mikubwa ambayo ameanzisha katika Mkoa wa Arusha, lakini pia ametujulisha kabla ya mwaka 2027 atakuwa amefanya jambo kubwa la kihistoria katika jumuiya hii, ambalo litaisaidia kuwa na uchumi mkubwa," alisema.

Kuhusu kamati ndogo nne zenye majukumu tofauti alizozindua, katibu mkuu huyo ambazo ni ya elimu, afya na mazingira, habari, utamaduni na hamasa, uchumi, mipango, fedha za uwekezaji na nidhamu na maadili alizitaka kutumia maarifa yao kulingana na majukumu waliyopewa kusaidia jumuiya hizo, katika masuala mbalimbali ya kiutendaji na kuleta mabadiliko chanya ndani ya jumuiya hiyo hasa uchumi.

Pia aliwaagiza viongozi wa jumuiya hiyo katika mikoa mingine, kuunda kamati hizo mara moja kwa kuwa tangu agizo hilo limetolewa ni Mkoa wa Arusha na Dar es Salaam pekee ndiyo wamekamilisha maandalizi ya kamati hizo.

"Mikoa ambayo hamjaunda kamati hizi ndogongogo ninawaagiza mfanye hivyo mara moja. Ninaupongeza sana Mkoa wa Arusha ambao wameunda kamati nzuri kuliko kamati tulizounda ngazi ya taifa," alisema.

Kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa, aliwataka wanachama wa jumuiya hiyo kuhakikisha wanaisaidia CCM kupata ushindi wa kishindo ambao utahakisi ushindi wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Awali akifungua kikao hicho, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Arusha, Mbise, alisema katika kipindi cha uongozi wake, atahakikisha jumuiya hiyo inajikwamua kiuchumi kwa kumiliki miradi mbalimbali.

# Mabosi watatu wasimamishwa kazi tuhuma ubadhirifu

**Na Oscar Assenga,** TANGA

HALMASHAURI ya Jiji la Tanga, imewasimamisha kazi watumishi watatu ili kupisha uchunguzi wa tuhuma zinazowakabili.

Jana Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Jiji hilo, Mussa Labani, alisema watumishi hao wamesimamishwa kuanzia Desemba 27 mwaka huu.

Waliosimamishwa kazi ni Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi na Miundombinu, Issa Mchezo, Mkuu wa Shule ya Sekondari Kiomoni, Fredrick Lubangulila na Mhandisi wa Majengo wa Jiji hilo, Baraka Noni.

Kwa mujibu wa Ofisa huyo, watumishi hao wanatuhumiwa kukiuka miongozo ya serikali ya ujenzi wa majengo ya SEQUIP (Mradi wa Uboreshaji Elimu ya Sekondari), kwa kuongeza gharama tofauti na ilivyoelekezwa na wizara na kuruhusu mikataba kuingiwa.

"Serikali ilitoa Shilingi milioni 584.2 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya Kata ya Kiomoni na ikatoa maelekezo na gharama za kila jengo. Mfano katika jengo la utawala, maelekezo ni lijengwe kwa shilingi milioni 77.7 lakini Mhandisi alitengeneza BOQ (makadirio ya ujenzi) ya shilingi milioni 140.

"Na Mkuu wa Shule na kamati yake wakaruhusu na kutoa mkataba wa ujenzi kwa gharama hiyo kubwa ya Sh.milioni 140, ambayo ni kinyume cha mwongozo."

Aidha, alisema pia ujenzi wa jengo lenye maabara ya kemia na biologia, maelekezo yalikuwa ni kujenga kwa gharama ya Sh. milioni 102, lakini gharama inayotumika ni Sh. milioni 150; uzembe huo umesababisha gharama za mradi kuongezeka kutoka Sh.milioni 584.2 na kuwa Sh. milioni 702.

Alisema: "Jambo hili limesababisha mradi kushindwa kujenga majengo mengine kama maktaba, chumba cha TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) na matundu ya vyoo".




Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba (katikati), akimpongeza Fatima Mwatime Nundu, ambaye ni mshindi wa kwanza wa samani za ndani katika kampeni ya Tisha na Tembocard Tukakiwashe Afcon inayoendeshwa na Benki ya CRDB. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## KKKT yasita kufungua milango kukaribisha wawekezaji UCB

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, amesema kanisa hilo linasita kufungua milango kwa wawekezaji wenye mitaji mikubwa, ili kuiongezea nguvu Benki ya Uchumi (UCB) kufikia takwa la kisheria la Benki Kuu ya Tanzania (BoT) la kufikisha mtaji wa Sh.bilioni 15.

UC inayomilikiwa na Dayosisi ya Kaskazini inahaha kufungua matawi nchi nzima, lakini kwa sasa inamtaji wa Sh. bilioni 12.78, na ina matawi pekee katika miji ya Moshi, Siha, Himo na Karatu.

Dk. Shoo, aliyasema hayo juzi katika Mji wa Moshi, wakati wa Mkutano Mkuu wana dayosisi hiyo kwa wajumbe wanaoishi nje ya Mkoa wa Kilimanjaro.

Vipaumbele vitano na mpango mkakati wa Dayosisi ya Kaskazini wa 2024/2028 ni kuwa na ukuaji endelevu wa kanisa, kuwa na uwezo endelevu wa kifedha na kiuchumi, kuwa na utawala bora na ufanisi wa uendeshaji.

"Kwa mujibu wa masharti ya BoT, ili benki yetu iweze kufungua matawi nchi nzima, inatakiwa kuwa na mtaji wa shilingi bilioni 15. Fedha hizi zinapatikana kwa uwekezaji na wadau.

"Ukweli ni kwamba, kupitia uwekezaji wa kimkakati, ipo fursa na kwa kweli kuna ushindani mkubwa wa wawekezaji wenye mitaji mikubwa kuweza kuwekeza fedha hizo kufumba na kufumbua.

...Dayosisi inaweza kusema, ruksa kufungua milango kwa wawekezaji wenye mitaji mikubwa lakini tangu awali, lengo lilikuwa sisi wenyewe kwanza, au wengine wanasema ukarimu unaanzia nyumbani."

Uwekezaji kupitia hisa, umewezesha UCB kukua kwa wastani wa asilimia 55 kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka 2023, ikiwa na mawakala zaidi ya 68.

## Waathirika Hanang' wapokea msaada vifaa vya ujenzi

**Na Mwandishi Wetu,** Hanang'

KAMPUNI ya Puma Energy Tanzania imekabidhi msaada wa vifaa vya ujenzi zikiwamo nondo 1,000, mabati 800 pamoja na saruji mifuko 600 kwa ajili ya kusaidia waathirika wa mafuriko ya matope yaliyotokea Kateshi wilayani Hanang' mkoani Manyara.

Vifaa hivyo vya ujenzi vya Sh.milioni 70 vimekabidhiwa jana kwa serikali kupitia Mkuu wa Wilaya ya Hanang mkoani Manyara, Janeth Mayanja.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa vifaa hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Hanang, Janeth Mayanja, aliishukuru kampuni hiyo kwa kutoa msaada wa vifaa vya ujenzi ambavyo kwa sasa ndivyo vinahitajika zaidi.


"Kwa niaba ya serikali nachukua nafasi hii kupongeza uongozi wa Puma Energy Tanzania kwa kufika Kateshi kutoa misaada wa vifaa vya ujenzi," alisema Mayanja.

Alisema kuwa msaada huo unakwenda kuongeza nguvu katika jitihada za serikali ambayo imeamua kujenga nyumba kwa waathirika baada ya kutokea mafuriko Desemba 3.

Aidha alisema msaada huo umekuja wakati muafaka kwani wamekuwa wakipokeza zaidi msaada wa mahitaji ya chakula na dawa, lakini kwa sasa wako kwenye hatua za mwisho kuanza ujenzi wa nyumba za waathirika.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Puma Energy Tanzania, Fatma Mohemed Abdallah, Meneja Uhusiano wa kampuni hiyo, Godluck Shirima alisema bodi ya wakurugenzi inayoongozwa na Dk.Selemani Majige, menejimenti ya kampuni inayoongozwa na Fatma Mohamed Abdallah, wafanyakazi na wadau wote wameguswa na tukio la mafuriko.

Alisema: "Hivyo viongozi wetu wakatuelekeza kuleta msaada huu wa vifaa vya ujenzi ili kuunga mkono juhudi na jitihada za serikali kuwajengea makazi waathirika waliopoteza makazi yao kwenye mafuriko".





# Uzazi waondoa uhai wa mwandishi wa habari Mwanza

**Na Waandishi Wetu**

KATIBU Msaidizi wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Mwanza (MPC), Brandina Aristides amefariki dunia na mtoto wake katika Hospitali ya Rufani Kanda Bugando baada ya kufanyiwa upasuaji wakati akijifungua.

Katibu huyo alifikwa na umauti Desemba 26 alipokwenda kujifungua katika hospitali hiyo, kwamba alifanyiwa upasuaji lakini hali yake kuwa mbaya na kupelekwa katika Chumba cha Uangalizi Maalumu (ICU), muda mfupi baadaye alifariki dunia.

Kwa mujibu wa taarifa za familia mwili wa Brandina na mtoto wake unatarajiwa kuzikwa leo eneo la Bulale, Buhongwa mkoani Mwanza.

Katika taarifa iliyotolewa juzi na Mwenyekiti wa MPC, Edwin Soko ilieleza kuwa MPC na tasnia ya habari imempoteza mtu muhimu aliyekuwa mstari wa mbele katika utekelezaji wa majukumu yake na kusaidia watu wengine.

"Uongozi wa Hospitali ya Bugando unaendelea kuweka taarifa vyema ili kuujulisha umma chanzo kamili kilichosababisha Brandina kufikwa na umauti wakati akijifungua hospitalini hapo," alieleza Soko.

Vifo vya uzazi vimeendelea kuwa tishio siyo tu kwa maeneo ya vijijini bali hata mijini kunakotajwa kuwa na huduma zote muhimu za afya ambapo katika kipindi cha mwaka 2021/2022 vifo vilikuwa vya uzazi mkoani Mwanza vilikuwa 114.

Mwaka 2022/2023 vilishuka hadi 96 kwa kila vizazi hai 100,000 hiyo ni kwa mujibu wa taarifa za ofisi ya Mkoa wa Mwanza.

Hata hivyo hivi karibu Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu katika mtandao wake wa X alitaja vifo vya wajawazito kuwa vimepungua kutoka 556 hadi 104 kwa kila vizazi hai 100,000 kitaifa.

Takwimu hizo za vifo vya uzazi kimkoa na kitaifa zimezua sintofahamu kwa waandishi wa habari mkoani hapa, huku wakitaka ukweli uwekwe wazi ili hatua za makusudi zichukuliwe.

Peter Salamba mwandishi wa gazeti la Mwananchi alisema: "kwa vyovyote na kwa lugha yoyote ile mama hastahili kupoteza uhai kwa kuleta uhai mpya, hivyo haikubaliki hasa katika kipindi hiki cha maendeleo ya teknolojia, uwekezaji na utaalam mkubwa katika sekta ya afya".

**Imeandaliwa na Neema Emmanuel na Vitus Audax (MWANZA)**




Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Shinyanga Mhashamu Liberatus Sangu, akiwa katika maandamano na watoto kupinga na kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya watoto mkoani Shinyanga, jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wakulima kuzalisha tumbaku tani 43,000 msimu 2023/24

**Na Halima Ikunji,** TABORA

TANI 43,000 za tumbaku zinatarajiwa kuzalishwa na wakulima mkoani hapa katika msimu wa kilimo kwa mwaka 2023/2024.

Hayo yamebainishwa juzi na Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Tumbaku Kanda ya Magharibi (WETCU 2018 LTD), Samweli Jokeya.

Alisema makisio hayo kuwa yanatokana na wakulima wanaotokana na vyama vya msingi vyenye wanachama 253.

Meneja Jokeya alitaja vyama hivyo vitakavyozalisha makisio ya msimu wa 2023/2023 ambayo ni kuanzia kilo milioni 42 hadi 54 kuwa vinatoka wilaya za Tabora, Uyui, Nzega na Sikonge.

Akizungumzia kuhusu pembejeo meneja huyo alisema hadi sasa asilimia 80 ya wakulima wamepata mbolea kwa ajili ya uzalishaji wa tumbaku kwa msimu ujao wa kilimo.

Aidha alitaja ongezeko la mvua zinazoendelea kunyesha kwa wingi kuwa miongoni mwa changamoto zinazokikabili kilimo hicho, huku zikiathiri suala la uwekaji wa mbolea shambani.

"Chama Kikuu cha Ushirika Kanda ya Magharibi tumeendelea kutoa elimu kwa wanachama wetu na kusisitiza wakulima wazingatie kilimo cha mazao ya chakula ili kujitosheleza kwa mahitaji pindi wanapokuwa wanavuna tumbaku na mazao mbadala kama tulivyowapa elimu na kuwaelekeza"alisema Jokeya.

Vilevile alitoa wito kwa wakulima hao wawe na kilimo cha zao mbadala tofauti na tumbaku, ili kuwa na uhakika wa chakula pamoja na biashara na kuacha kutegemea zao hilo kwa asilimia zote.

# Mvua yaharibu nyumba 12, mamia wakosa makazi

**Na Benny Kingson,** TABORA

MVUA iliyonyesha kwa zaidi ya saa tano usiku wa kuamkia Desemba 27 mwaka huu katika mtaa wa Kombamasai Kata ya Malolo Manispaa ya Tabora imesababisha uharibifu wa nyumba 12, huku nyingine zaidi ya 150 zikizingirwa na maji.

Mvua hiyo iliyonyesha kuanzia saa nane usiku hadi asubuhi ilisababisha pia uharibifu wa mali mbalimbali za wananchi.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufanyika kwa tathimini ya madhara ya mvua hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Tabora Luis Bura alisema ni nyumba 12 ziliharibiwa na mvua, huku 150 zikizingirwa na maji na kusababisha uharibifu wa mali mbalimbali za wakazi wa maeneo hayo.

Aidha alisema hakuna kifo kichotokana na mvua hizo, akiwataka wataalamu wa barabara kuweka nguvu katika kurekebisha miundombinu ya mitaro iliyozibwa na uchafu uliokusanywa na mvua hizo.

"Mvua kubwa imenyesha katika maeneo mbalimbali na kusababisha maji kujaa katika kata hii ambapo ni kawaida lakini kwa kipindi kipindi hiki yalikuwa mengi kupita kiasi yakisomba taka zilizoziba mitaro iliyopo na kuingia kwenye makazi ya watu," alisema Bura. Alitoa ombi kwa wakazi wanaoishi katika maeneo ya miinuko kuwasaidia ambao makazi yao yamezingirwa na maji makazi ya muda wakati wakisubiri maji yaliyowavamia yakauke.

Awali Mwenyekiti wa mtaa wa Kombomasai, Doto Rajab aliliambia Nipashe kuwa baadhi ya mali za watu zilizoharibiwa kuwa ni pamoja na magodoro, vyakula pamoja na vitu mbalimbali vya ndani vikiwemi vifaa vya umeme.

Pia alitaja miundombinu ya barabara kuharibiwa na mvua hizo hali iliyositisha kuendelea kwa shughuli za kiuchumi katika manispaa hiyo.

Kadhalika akitaja kutokuwepo kwa mitaro ya kusafirisha maji kutokana na barabara zinajengwa bila kuwekewa mitaro imara hali inayosababisha mitaro kuziba na maji kuhamia kwenye makazi.

Mwenyekiti huyo alisema amekuwa akiwahamasisha wakazi wake kujitengenezea mitaro ya kuchepusha maji ya mvua ambayo yanatokea maeneo mbalimbali kila wakati, lakini jitihada zao wakati huu zimegonga ukuta kutokana na mvua hizo kuwa kubwa.

Yahaya Hamis mkazi wa eneo hilo alisema: "Tunaomba serikali ifanyie ukarabati wa mitaro kwa kuijengea kwa mawe ili iruhusu maji kwenda nje ya mji na makazi ya watu maana hili tatizo limekuwa la mara kwa mara licha ya leo (juzi) kuonekana kuwa kubwa zaidi".



Ukurasa 12

IJUE HIFADHI YA TAIFA MTO UGALLA...
Ina miaka minne, utajiri kibao, watalii wakuu wazawa




**Bila televisheni, kumbe hakuna michezo kwetu!**

Ukurasa 13



# Dk. Samia alipowapa darasa viongozi Afrika uwekezaji unavyopitia vijana

## •Asema mtoto akizaliwa kazi yake inaanza

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, katika dira yake kiuchumi anasema uwekezaji unahitajika kuchochea maendeleo ya Afrika na zaidi ya muongo mmoja sasa, bara linaimarika kiuchumi kwa kasi katika sekta tofauti, ikiachana na misamiati ya kale inayowakebehi.

Anafafanua, harakati mbalimbali zimefanyika kulikwamua bara kutoka kwenye uchumi tegemezi, sasa likitumia rasilimali zake kujiletea maendeleo.

Dk. Samia anakiri baadhi ya nchi na kanda, maendeleo hayajafika katika sura ya kujenga uchumi jumuishi au hata kuchochea uzalishaji ajira mpya, hususan vijana.

Pia, akataja Afrika inakabiliwa na changamoto kama za uhaba wa chakula, kukosekana ajira, umasikini na hata kukosa usawa wa kijamii.

"Ni wazi kuwa bara letu bado linahitaji mageuzi makubwa katika nyanja zote muhimu za uzalishaji na maendeleo," anatamka Rais Dk. Samia.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akizungumza katika mkutano uliohusu viongozi wa Afrika. **PICHA: MTANDAO.**

**SAFARI YA KUSONGA 2063**

Anataja lengo la kufikia mwaka 2063, Afrika ina malengo saba: Mosi, anajikita katika hoja kuwa na uchumi jumuishi; bara kuwa na utangamano kisiasa wenye fikra jumuishi na mwelekeo wa kimapinduzi.

Vilevile anataja misingi ya utawala bora, demokrasia, haki za binadamu na utawala wa sheria; hali kadhalika maendeleo yanayotokana na watu wakitumia vipaji vyao, hususan wanawake na vijana wakilea vilivyo watoto.

Anasema kwa sasa Afrika ndio bara lenye vijana wengi zaidi, takwimu zikionyesha ifikapo mwaka 2050, itatoa nchi 10 zenye idadi kubwa zaidi ya vijana duniani.

Kwa mujibu wa Baraza la Uchumi Duniani, zaidi ya asilimia 60 ya watu Barani Afrika ni vijana chini ya miaka 25, ikikadiriwa kufika mwaka 2030, Afrika itakuwa na asilimia 42 ya vijana wote duniani.

Hapo anafafanua kwa tafsiri ya kidemografia, inakuwa habari nzuri, vilevile mbaya; maana yake kuna tija iwapo tutawekeza kwenye rasilimali watu na kuhakikisha kuwapo afya na elimu bora ya stadi za kimaisha, kama mfano wa bara la Asia sasa.

"Tusipofanya hivi, tutaongeza idadi ya vijana wasio na ujuzi, wasioajirika na wanaokosa mwelekeo wa maisha, hali itakayopelekea vijana hao kujiingiza kwenye vitendo viovu vya kihalifu na uvunjifu wa amani..." anasema

Dk. Samia anamnukuu Mwalimu Julius Nyerere, alipohutubia kikao cha kimataifa jijini New York, Marekani akinena: "Maendeleo ni watu. Watu ndio walengwa waanzilishi na wanufaika wa chochote kinachoitwa maendeleo."

Hapo akarejea takwimu zinazoonyesha ifikapo mwaka 2050, Afrika itatoa nchi 10 zenye idadi kubwa zaidi ya vijana duniani.

Dk. Samia anahimiza uwekezaji katika rasilimali watu unaangukia kuhakikisha tangu mtoto anapozaliwa, akimaanisha upatikanaji lishe bora na chanjo stahiki, ili kuondoa udumavu ambao mara nyingi, unapunguza kiwango cha uelewa na uwezo wa kusoma kwa watoto.

Rais Dk. Samia anakumbusha hapo kwamba kunapaswa jamii ikawekezwa misingi bora ya elimu ya awali inayomuandaa mtoto kimwili, kiakili, kiisimu, kijinsia, kiubunifu na kiakili-hisia.

Pia, Dk. Samia anataja kwamba ili elimu husika ikatoe matokeo chanya, ni lazima kuwapo mitaala darasani inayokidhi matakwa ya soko la ajira.

Katika hilo anatoa mfano wa kuwapo mapinduzi ya nne ya viwanda, yanayoilazimisha jamii kwenda na wakati na haipitwi na teknolojia mpya.

"Mapinduzi haya ya nne ya viwanda yameleta mabadiliko makubwa katika sekta zetu za afya, elimu, biashara, teknolojia na mahusiano na mwingiliano wa kijamii, pamoja na usafiri na usafirishaji," anasema, akikumbusha wajibu wa Afrika kuhakikisha haiachwi nyuma.

Hapo Dk. Samia anatetea hoja yake kwa kumnukuu Mwasisi wa Taifa Huru la Afrika Kusini, Mzee Nelson Mandela, aliyetamka "elimu ndio silaha yenye nguvu zaidi inayoweza kutumika kubadilisha ulimwengu"

Kajengea msisitizo hoja yale akisema, kuna haja ya kutengwa fedha za kuboresha lishe na huduma za afya ya uzazi wa mama na mtoto na kuwaanzishia vituo vya elimu ya awali.

Pia, ni kufanya mapitio na maboresho ya sera ya elimu, mitaala na programu za mafunzo, ili ziendane na mazingira, pia mahitaji ya sasa ya maendeleo.

Maeneo mengine katika hoja yake iliyo na sura na mipango ya Uchumi, Dk. Samia akakumbusha haja ya kuwa na uanzishwaji Mfuko wa Kusaidia Kaya Masikini, nchini ukiwapo Tanzania Social Action Fund

Inaendelea Uk 12

UCHUMI

IJUE HIFADHI YA TAIFA MTO UGALLA…

# Ina miaka minne, utajiri kibao, watalii wakuu wazawa

**Mwandishi Wetu**

KUNAPOTAJWA hifadhi ya taifa, maana yake kuna vivutio mbalimbali vya kipekee kitaifa. Hapo ndiko panapobeba maana hata kwa Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla, mkoani Tabora, huku ukiwa na upande mwingine mkoa kama Katavi.

Moja ya sifa zake, kundi kubwa la watalii mahali hapo ni watalii wazawa, huku sehemu ya kivutio chake ni mandhari ya Mto Ugalla, unaopatikana ndani yake, ukinakishiwa na mandhari ya asili ndani yake.

Hapo kuna utajiri wa misitu, miti jamii ya miombo na uwanda chepe wa wazi wenye sehemu ya ardhi oevu, unaotambuliwa na jumuia ya kimataifa ya uhifadhi.

Vilevile, una kivutio cha ushuhuda wa makundi makubwa ya wanyama wakiwamo viboko, nyati, simba, chui, tembo, pundamilia na twiga, kukiwa kumepambwa na maji mengi ya Mto Msima na mto mkubwa wa Ugalla, unaobeba jina la hifadhi.






Mandhari tofauti ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

Wanyama wengine ni kama swala, pala, tandala, Hifadhi ya Mto Ugalla yenye utajiri wa ndege na wa jamii mbalimbali na ilianzishwa mwaka 2019, kwa tangazo la Serikali Namba 936 ikiwa na ukubwa eneo la kilomita za mraba 3,865.

Ilianzishwa kwa kuunganishwa Msitu wa North Ugalla wenye ukubwa wa kilomita za mraba 2,054 uliokuwa chini ya Wakala wa Huduma za Mistu Tanzania (TFS) na sehemu ya Pori la Akiba la Ugalla, lenye kilomita za mraba 1,811, chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA). kongoni, pofu, mbwa mwitu, pongo, ngiri, nyani na nguruwe mwitu.

**UMAARUFU WAKE**

Ni hifadhi iliyoko magharibi mwa Tanzania, katika mkoa wa Tabora, ni ya sita kwa ukubwa kati ya hifadhi 21 na inapakana na wilaya ya Urambo kwenye vijiji 10 huku Wilaya ya Kaliua ikipakana na vijiji tisa.

Pia, upande mwingine inapakana na Pori la Akiba la Ugalla, mkoani Katavi na Mkuu wa hifadhi hiyo, Kamishna Msaidizi Lomi Ole Meikasi, anafafanua kuna utajiri wa miti, wanyama wengi, mvua za kutosha na mito yenye maji mengi.

Kiikolojia anaitaja kuwa kiunganishi cha ushoroba wa wanyamapori wa Ugalla-Moyowosi- Kigosi, mapori ya akiba ya Rungwa, Rukwa na Luganzo-Tongwe na Hifadhi ya Taifa ya Katavi.

Meikasi anasema, hifadhi hiyo ni chanzo cha eneo lenye ardhi oevu la Malagarasi-Moyowosi, ikiwa ni miongoni mwa maeneo yanayotambuliwa kimataifa yaliyopo nchini.

Vilevile, kunatajwa kuwapo hazina kubwa ya ndege mbalimbali, wakiwamo yangeyange, mbuni, njiwa, kwale na shoebill stork, wenye tabia ya kuhama umbali mrefu kutoka eneo moja hadi lingine.

Meikasi anasema, Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla, inafikika kirahisi, kwa kutumia usafiri wa barabara, ndege na treni ya Tabora-Mpanda inayopita kando yake.

Anasema, mahali hapo kumejengwa miundombinu ya barabara nyingi hifadhini, zenye jumla ya kilomita 496, ambazo zimesaidia kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea.

Hapo mhifadi huyo anasifu jitihada za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kutangaza vivutio vya utalii nje ya nchi kupitia sinema iitwayo 'The Royal Tour', sasa zimesaidia kuongeza idadi ya watalii wanaofika Ugalla.

Pia, anasema wanatarajia kujenga ndani ya hifadhi maeneo zaidi ya kupumzikia wageni, nyumba za kulala wageni na kuweka boti itakayotumika kutembeza watalii kipindi cha mvua, kupitia Mto Ugalla na kujenga barabara zinazopitika muda wote.

Anafafanua, hiyo inatokana na hali halisi ya ardhi mahali hapo, kipindi chote cha mvua, njia na maeneo mengi hifadhini Ugalla, hubaki oevu, hata kuleta ugumu wa usafiri kirahisi.

Mhifadhi Mkuu Meikasi, anatoa wito kwa wawekezaji wa ndani na nje, kujenga hoteli za kitalii kando ya hifadhi hiyo mpya, ili kuendana na kasi ya ongezeko la watalii.

Ofisa Msaidizi wa Kitengo cha Utalii, Mathayo Melau, anasema watalii wa nje waliotembelea hifadhi hiyo katika kipindi kuanzia mwaka 2020, hadi Novemba mwaka jana ni 40, huku wa ndani wako 1,026.

Anasema katika picha ya jumla, watalii wameongezeka kutoka mtalii mmoja wa nje mwaka 2020 na idadi kufika 24, kwa kipindi cha mwezi Julai mwaka huu, hadi mwezi uliopita.

Melau anasema watalii wa ndani nao wameongezeka kutoka mmoja mwaka 2020 hadi 558 katika kipindi cha kuanzia Julai hadi mwezi uliopita.

**CHANGAMOTO ZILIZOKO**

Kuhusu changamoto zao, Meikasi, anafafanua kuwa, pamoja na kuwapo ongezeko la watalii na maboresho yaliyoko, bado kunakabiliwa na matatizo kama ya ujangili, uvamizi wa mifugo, uvuvi haramu na shughuli za kibinadamu kuwaingilia.

Mkuu wa Kitengo cha Sheria na Ulinzi Mkakati wa hifadhi hiyo, Erick Kimario, anaeleza katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2023, jumla ya majangili 216 na mifugo 2,052 ilikamatwa, huku watuhumiwa wakifikishwa mahakamani.

Kimario anasema, wameimarisha ulinzi kwa kufanya doria za miguu na kutumia ndege, pia magari hifadhini kote, lengo ni kukomesha ujangili na uvamizi wa mifugo, huku wakitoa elimu wananchi wanaoishi jirani.

Vilevile, anasema wanafanya doria za pamoja na majirani zao, TAWA na TFS kukabili vitendo hivyo, hali inayosaidia kuzalisha matokeo chanya.

**MIKAKATI KUKUZA UTALII**

Melau, anasema Hifadhi ya Mto Ugalla ina mikakati mingi ya kukuza utalii wake, ikiwamo kuitangaza kupitia vyombo vya Habari, ndani na nje ya nchi kupitia maonyesho mbalimbali ya kimataifa.

Vilevile anasema, wameanzisha kampeni ya 'mlango kwa mlango' umma unaoishi kando ya hifadhi, wafanyabiashara, taasisi za umma, binafsi, vyuo, shule za sekondari na msingi mkoani Tabora.

Anasema wanafanya hilo, pia kwa kushiriki kwenye maonyesho ya biashara, sherehe na matukio ya kitaifa na kikanda, Mbio za Mwenge wa Uhuru na mitandao ya kijamii.

**MIRADI UJIRANI MWEMA**

Mhifadhi Idara ya Uhusiano wa Jamii wa Hifadhi hiyo, Sadick Mohamed, anasema katika kuboresha uhusiano wa hifadhi na wananchi wanaoishi kuzunguka, wanawapa mafunzo kujenga uelewa wake kwa umma.

Mohamed anafafanua kwamba, njia wanazotumia kutoa elimu hiyo zinajumuisha mikutano ya hadhara, vikao, semina, maonyesho ya ndani na nje mkoani Tabora.

Pia, anataja kuanzia mwaka 2020 hadi mwaka jana, wameshiriki vikao 213 vya elimu ya uhifadhi vimefanyika na kuwashirikisha watu 38,244.

Mohamed, anasema mkakati wao katika mwaka wa fedha wa sasa 2023/2024 wanatarajia kutekeleza miradi miwili ya ujirani mwema yenye jumla ya thamani ya Sh. 296,049,719.

Anaitaja kuwa ni kujenga jengo la Wagonjwa wa Nje (OPD) kwenye Kituo cha Afya cha Kata ya Ukumbisiganga wilaya ya Kaliua, wenye thamani ya Sh. 250,418, 694 na kujenga choo chenye matundu 24, katika Shule ya Msingi Lunyeta, iliyopo kijijini Kangame, kata ya Nsenda wilaya ya Urambo wenye thamani ya Sh. 45,631,024.

Aidha, hifadhi imeendelea kutoa misaada mbalimbali kwa watu wanaoishi kando ya hifadhi, ikiwamo viti na meza za

walimu kwa Shule ya Sekondari Ushokola wilaya ya Kaliua, na 'printa' kwa Shule ya Sekondari Ukumbisiganga, wilaya ya Kaliua vyote vikiwa na thamani y ash 3,000,000.

Katika hilo, Kaimu Mtendaji wa Kijiji cha Usinga, Prosper Sakaya, anaishukuru Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla kwa kuwapatia misaada ikiwamo elimu ya uhifadhi kupitia Kitengo cha Ujirani Mwema.

"Tunaishukuru sana hifadhi ya Mto Ugalla wametusaidia sana kwa kutupatia elimu ya uhifadhi na misaada mbalimbali," anasema Sakaya.

Anasema kwa uongozi wa Kijiji, pia umekuwa ukitoa elimu ya uhifadhi kwa wananchi, kuacha kuingia ndani ya hifadhi kufanya ujangili na shughuli nyingine za kibindamu.



## DK. SAMIA ALIPOWAPA DARASA VIONGOZI AFRIKA UWEKEZAJI UNAVYOPITIA VIJANA

**INATOKA UK. 11**

**(TASAF).**

Katika ufafanuzi mfupi wa TASAF nchini, tangu mwaka 2000, zaidi ya kaya milioni moja zimenufaika na zaidi ya miradi 731 ya miundombinu ya elimu, afya, maji safi na salama, kilimo na mazingira; njia za usafiri na usafirishaji zimetekelezwa.

**MTAJI ELIMU**

Eneo lingine Dk. Samia analitaka liwe katika fikra jumuishi Afrika ni kuanzishwa programu ya elimu bila malipo kwenye ngazi za elimu ya awali, msingi na sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita.

"Uwekezaji kwenye elimu ya ufundi na mafunzo ya amali, yaani 'Vocational Education and Training', ikiwa pamoja na kutoa ujuzi bobezi ili kuongeza tija, ushindani na uwezo wa ndani katika kutumia maliasili za nchi yetu," anatamka.

Ni mtazamo unaoendana na uwezeshaji vijana kiuchumi kupitia mikopo inayotolewa na halmashauri kwa vijana, asilimia nne mfano hai ni inayotekelezwa.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Bila ya kuwa na televisheni, kumbe hakuna michezo kwetu!






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

ZAMANI tukiwa shule za msingi, tulikuwa na vipindi vya PE (Physical Education) kuanzia darasa la kwanza mpaka la saba na ilikuwa lazima kuhudhuria kipindi cha PE, ambacho kilikuwa cha michezo.

Hiyo ilikuwa mbali na mchakamchaka tuliokuwa tukikimbia asubuhi kabla hata ya kufanya usafi wa mazingira na kujipanga kukaguliwa, kabla ya kuingia madarasani.

Lengo ni kuwaamsha wanafunzi na kuwatia ukakamavu, ili kufuatilia vema masomo darasani, hakika mchakamchaka na PE vilituchangamsha sana wanafunzi na hatukusinzia kwenye vipindi.

Kwa kweli tulikuwa wakakamavu na katika mashindano ya michezo, tulifanya vizuri, kwani hakukuwa na magonjwa ya mara kwa mara na hasa, pia kutokana na chakula tulichokula shuleni-bulga na hata majumbani-ugali.

Enzi hizo uji ulitawala sana, si nyumbani lakini hata shuleni, kabla haujaja utamaduni wa kunywa chai. Pia. hatukuwa na chipsi, kwani kama si kiporo cha ugali basi tulifakamia viazi au mihogo.

Leo hii ukila kiazi au muhogo unaonekana masikini, ila ukikutwa na chipsi unaonekana kutoka familia ya kitajiri, hakuna PE wala hakuna mchakamchaka shuleni.

Vivyo hivyo, hakuna mashindano ya michezo mingi kama zamani, ambayo tulishindana riadha na michezo ya mpira, ambayo tulishindana kukimbia mbio ndefu na fupi.

Pia, tulishindana kuruka chini na juu, kutupa kisahani na tufe, kurusha mkuki na hata kuvutana kamba. Shule na shule zilishindana hata katika soka na netiboli, pia mpira wa wavu na kikapu.

Katika mashindano hayo, ndiko tulikopata wakimbiaji mashuhuri kama kina Mwinga Mwanjala (mnaokumbuka) na wengine waliotuwakilisha, katika mashindano ya kimataifa na kuliletea taifa sifa.

Serikali ilipofumbua macho, ikaja na michezo ya shule za msingi, sekondari na vyuo na hivyo kupata wanariadha wengi, lakini hata wanasoka wengi na michezo mingine.

Hata mawaziri wa michezo enzi hizo waliitendea haki, kabla hajaja mmoja aliyekuwa na maono tofauti, akaondoa michezo shuleni, eti akitaka watu wajikite darasani zaidi.

Waziri huyo akaua michezo shuleni na taifa, likawa kama halina mwenyewe kwenye michezo, lakini kama kawaida akawa anatazamwa tu huku tukimwachia Mungu atuamulie mwenyewe la kufanya.

Tuliendelea kusuasua hivyo mpaka alipokuja waziri mwingine aliyeona umuhimu tena wa michezo shuleni akairudisha, baada ya kuwa tumejikongoja sana nyuma ya mataifa mengine yakiwamo ya jirani.

Tukaibuka, lakini tumechelewa sana na kung'ang'ania humo, kwa kuwa na wizara ikibadilishwa mara iwe na michezo mara ichanganywe na elimu, hata mwelekeo ulikuwa nini.

Ni mpaka hapo zilipoibuka televisheni zikaanza kurusha michezo mbashara hususan soka, riadha, ndondi, netiboli, wavu, kikapu na mingine, ndipo sasa tunaona nafuu kuwa tunapiga hatua katika michezo.

Hizi televisheni zimetuondolea tongotongo zilizotokana na usingizi mzito tuliolala kwa muda mrefu na kuona kama michezo si kitu katika jamii.

Leo ligi yetu ya soka wanaume inashika nafasi ya tano Afrika. Ligi hii inatazamwa kitaifa na kimataifa katika televisheni zetu.

Hiyo imewezeshwa na uwekezaji mkubwa wa vyombo hivyo vya habari nchini, hivyo kustahili pongezi hata kuliko wizara husika ambayo haina kubwa la kuonyesha.

Muktadha uliopo, pia umefanya wenye timu zao za soka daraja la kwanza kujikamua na kusajili wachezaji wenye uwezo na sifa kubwa Afrika na kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa.

Nani wa kuigusa Tanzania leo? Katika kusaidiana na televisheni hizi, serikali kupitia Wizara za Elimu na Michezo, ihakikishe inarejesha vipindi vya michezo shuleni hususan PE na mchakamchaka, ambako itaweza kupata wanamichezo wengi.

Tusijisahaulishe kuwa hata katika michezo hususan soka, wachezaji wengi wanaoiletea sifa nchi ni wa kigeni. Wa kwetu ni wachache sana, lakini kwanini iwe hivyo, wakati nchi ina watu zaidi ya milioni 60 sasa huku ikijigamba ni tajiri?

Ni kwa sababu serikali haina mipango madhubuti ya kuhakikisha michezo inajengwa na kukua kama ilivyo kwa mataifa mengine.

Wachaguliwe watu mwafaka wanaojua michezo na maana yake, ili waisimamie na watengeneze vijana watakaolisaidia taifa katika nyanja hizo.

Hivi sasa tuache kuwa na vijana legelege wasiofanya michezo na badala yake wanakalia kufakamia machipsi na kutarajia kufanya mazoezi kwenye matamasha na jogging. Televisheni zikifa, nalo Taifa litakufa kimichezo. Mungu tubariki!

FEDHA

BAADA YA WAKULIMA KUUA USHIRIKA NA KUKIMBIA…

# Hali mbaya yawakabili warithi, mashamba ya tumbaku yakwama, benki zagoma kuwakopesha

**Na Neema Sawaka, KAHAMA**

WAKATI serikali inaendelea na mikakati ya kuboresha maisha ya wakulima nchini, wilayani Kahama kuna sintofahamu kwa baadhi ya wakulima wa tumbaku kutoka vyama vya msingi 13, wanaodai kupewa vyama vyenye madeni zaidi ya Sh. bilioni 3.7 yaliyotelekezwa kwa miaka 11 iliyopita.

Pia, kuna sura nyingine benki nazo zinasita kutoa mikopo kwa vyama hivyo vya ushirika, kwa madai vinatakiwa kulipa fedha hizo za madeni.

Madai ya baadhi ya viongozi wa vyama hivyo vya msingi (AMCOS), katika msimu wa mwaka jana, 2022/2023, walilima tumbaku kupitia vyama vya pamba na wao walikuwa na vyama vyao vilivyokuwa vinalima pamba.

Inaelezwa, baadaye wakasajiliwa kulima tumbaku kwa majaribio na Mrajisi wa Vyama vya Ushirika mkoa wa Shinyanga na kwa mujibu wa sheria wakalima zao hilo la tumbaku msimu uliopita wakifanya vizuri kwa kulipa madeni yote ya wakulima na mikopo ya benki.

Aidha, wanasema pamoja na kufanya vizuri, vyama vyao vilifutwa kwa madai ya kufufua vyama vya zamani vyenye madeni vilivyokimbiwa na viongozi wake, ambavyo ushirika wake ulishasambaratika na waliokopa hayo madeni ni wengine .

Inaelezwa vyama hivyo wakapewa wakulima kwa masharti ya kuviendeleza kwa kulipa madeni yanayodaiwa yaliyotelekezwa zaidi ya miaka 11 sasa.

Akizungumza kwa niaba ya viongozi wengine, mwenyekiti wa Bukomela Amcos, Charles Nkwabi, analalamika chama chake cha msingi alichopewa kinadaiwa Dola za Marekani 155,000 (Sh.390,522,500), zilizokopwa na viongozi wengine, pia wakulima wengine, katika ushirika uliokwishasambaratika.

Nkwabi anahoji sababu za wao kupewa madeni ya vyama ambayo hawahusiki navyo:“Suala hilo linarudisha nyuma juhudi za wakulima za kujikwamua kiuchumi ambao wamelazimishwa kulipa madeni ambayo hawajayakopa, kwa kupewa vyama vyenye madeni.”

Nkwabi anasema kwa sasa benki zimegoma kutoa huduma ya mikopo ya pembejeo, ikiwamo fedha za kununulia mbolea, viuatilifu ujenzi wa mabanio ya kuni, zinazowezesha wakulima kuendesha kilimo, zikipewa masharti zitaendeleza mikopo, pale fedha zilizokopwa miaka 11 iliyopita zitarejeshwa.



Wakulima wa tumbaku Shinyanga wakiwa kwenye kikao kinachowahusu.

Magema Machiya, mkulima wa tumbaku kutoka katika Halmashauri ya Ushetu, anadai kutwishwa vyama vyenye madeni na mfu kwa miaka mingi, kuwaonea.

Pia, anasema kilimo cha tumbaku sasa kina gharama wasiyoimudu na inakuwa vigumu kwao kufikia malengo na makisio ya uzalishaji shambani.

Kuhusu hali inayoendelea, anafafanua: “Mpaka sasa hatujaweka mbolea kwenye mashamba ya tumbaku , tumekosa pembejeo, ikiwamo mbolea, viuatilifu na kuni, fedha za kutengenezea majiko ya kuchomea tumbaku hatuelewi hata fedha za kugredi zao hili zitatoka wapi kutokana na kukosa mikopo kutoka kwenye benki “.

Mkulima wa tumbaku, Scolastika Makaji, analalamika kilimo hicho kinaenda na kalenda ya muda, hivyo upandaji tumbaku unatakiwa ukae siku saba, ifuate mbolea na baada ya siku 10 linakuja lingine.

Hapo anasema kwa sasa walioanda tumbaku tangu mwezi Oktoba na wengine Novemba, hawajapata pembejeo kwa wakati, hali inayowaweka hatarini kukosa mavuno waliyokuwa wakiyategemea.

“Mheshimiwa Rais Samia, tunatambua unasikiliza kilio cha wananchi wako na ni msikivu fanya ziara mkoa wa Shinyanga hasa wilaya ya Kahama ujionee wakulima wako wa mkoa wa ki -tumbaku wa Kahama wanavyonyanyaswa, kwa kulazimishwa kujiunga kwenye ma vyama yenye madeni, huku vyama vyao visivyokuwa na madeni vikifutwa...”

Mwingine, Stephano Mhanganya, wao kupewa vyama yenye madeni anautaja ni ‘ukandamizaji’ na ‘unyonyaji’ kumlipia mtu deni ambalo hawakulikopa ,waliopewa chama hicho chenye madeni wanalazimishwa kulipa.

Anafafanua, alitakiwa ofisa ushirika mhusika awasaidie kuunda vyama vipya visivyo na madeni, akilalamika ni suala litakalosababisha wakulima kutofikia malengo yao na kushusha uzalishaji, kwa kuwavunja moyo .

**KUTOKA WADAU TUMBAKU**

Kampuni ya Ununuzi wa Tumbaku Mkwawa, inasema imepata taarifa hiyo wiki iliyopita ya changamoto ya vyama vyenye madeni kukosa pembejeo na mikopo kutoka benki.

Pia, kunatajwa kuwapo mawasiliano na makao makuu ya kampuni hiyo, kuona namna ya kuwasaidia wakulima hao kuendesha kilimo hicho kupitia vyama vyao vya msingi.

Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika Wilayani Kahama, Abdul Mauga, anasema walifanya makubaliano na benki za Azania, CRDB, na NMB zihudumie AMCOS hizo 13.

Mtazamo ni kutolewe mikopo ya pembejeo na kuni na mingine inayotolewa kwa ajili ya kuendesha kilimo hicho, kama ambavyo zimetoa mikopo kwa amcos zingine zisizo na madeni .

Meneja wa Benki ya CRDB Kanda ya Magharibi Jumanne Wagana, anafafanua kuwa wao kama benki wanatoa mikopo ya pembejeo, zikiwamo mbolea mbegu ,viuatilifu pamoja na fedha za kujengea mabanda , kuandaa kuni vibarua na kugred zao hilo na zinatoka kwa awamu mbalimbali.

Anasema, vyama vyote vilivyolaza madeni ya muda mrefu huko nyuma, hawawezi kuwakopesha na hawakopesheki na hawawezi kutoa mikopo mingine mipya kwa amcos zilizolimbikiza madeni muda mrefu hilo ni kwa benki zote na ni maelekezo kutoka benki kuu.



Mkulima wa tumbaku Kahama, akiwa kazini. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Meneja huyo anafafanua: “ tunatoa ushauri kwa wakulima na wanachama wa amcos lazima wajue mali na madeni ya chama kabla hawajajiunga, kwani wakijiunga kwenye vyama vyenye madeni, watarithi madeni ya vyama hivyo.

“Kama ni wanachama wapya, waanzishe vyama vipya vya msingi visivyo na madeni na kuongeza kuwa ‘amcos’ ndio zinaleta maombi benki na wao wanatoa vigezo vya kupewa mikopo.”

Kwa upande wake, Ofisa Ushirika wa mkoa wa Shinyanga , Hilda Boniphace, anaiambia Nipashe ,kwa njia ya simu, kuwa lengo la mkoa ni mpango wa kufufua vyama vya msingi na kulipa madeni ya benki yaliyosababishwa na wakulima kuviua vyama na kukimbilia vyama vingine.

Hilda anasema, ni hali itakayowaondoa wakulima wachache wanaoua vyama kila mwaka na ndio maelekezo ya mkoa mzima wa Shinyanga.





# DUWASA yafanikiwa uondoshaji majitaka mjini, pembezoni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), Aron Joseph, ameishukuru serikali kwa kuipa kipaumbele mamlaka hiyo kutatua tatizo la upatikanaji wa maji na uondoshaji wa majitaka mjini na maeneo ya pembezoni.

Alitoa pongezi hizo jana mkoani hapa wakati wa kutoa taarifa ya hali ya upatikanaji maji wakati wa kikao cha kamati ya ushauri ya Mkoa wa Dodoma.

Alisema serikali imekuwa ikisaidia DUWASA katika kutatua kero hiyo ambapo kwa sasa miradi mingi inatekelezwa na iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

"Kwa sasa wakazi wa Mji wa Dodoma wanapata huduma ya majisafi na salama takribani asilimia 91 kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na migawo," alisema.

Alisema, miundombinu ya kusafirisha maji katika vyanzo vya visima virefu vya bonde la Makutupora eneo la Mzakwe na vyonzo vingine vidogo ni lita milioni 68.6 wakati mahitaji ni lita milioni 133.4 kwa siku, hivyo upungufu ukiwa ni lita milioni 64.8 kwa siku.

Akizungumzia miradi inayotekelezwa, alisema ni pamoja na mradi wa majisafi Nzuguni ambao utaongeza upatikanaji wa maji kwa asilimia 11.7, hivyo kutoka lita milioni 68.6 za sasa hadi lita milioni 76 kwa siku.

Alisema awamu ya kwanza ya mradi huo umefikia asilimia 96 na unatekelezwa kwa Sh. bilioni 4.391, huku awamu ya pili itahusisha uchimbaji wa visima vitano kwa Sh. milioni 220 na uchimbaji wa kisima kirefu kwa Sh. milioni 570.

Alisema mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria, Wizara ya Maji iko katika hatua za mwisho za majadiliano na mhandisi mshauri.

Pia mradi wa ujenzi wa Bwawa la Farkwa ambao ukikamilika utatosheleza upatikanaji wa maji Dodoma mjini na maeneo ya pembezoni na utatumia Dola za Marekani milioni 135.8 sawa na Sh. bilioni 312. 08.

Alisema pia DUWASA inatekeleza mradi wa kupitia usanifu na kusimama ujenzi wa mtandao wa majisafi na uondoshaji wa majitaka katika mji wa Magufuli na mradi wa uchimbaji wa visima 10 pembezoni mwa mji.

Alisema pia mradi wa majisafi Nala-Itracom utakaohusisha uchimbaji visima vitatu kwa Sh. milioni 520.376 na mradi wa majisafi Nala DTC ambao una gharimu Sh. milioni 425.879 umefikia asilimia 20 kwa sasa.

Alisema mradi mwingine ni wa ukarabati kwa lengo la kuongeza wingi wa maji wa chemchemi ya Sagara katika mji wa Kongwa ambao unagharimu Sh. milioni 129 na umefikia asilimia 90 ya utekelezaji.

Pia mradi Michese Nzinje ambao unahusisha usambazaji maji katika mtaa wa Nzinje kwa gharama ya Sh. milioni 125 na umefikia asilimia 96 na mradi wa maji wa Mkonze Muungano A ambao unagharimu Sh. milioni 92.

Alisema mradi wa maji wa Ndurugumi-Kibaigwa unaogharimu Sh. milioni 805 umefikia asilimia 93 na mradi wa maji katika miji 28 wa Chamwino ambao utanufaisha wakazi 44,269.

Kuhusu uondoshaji wa majitaka, alisema tayari DUWASA imekamilisha kulipa Sh. milioni 611 kama fidia kwa wananchi wanaopisha eneo litakalojengwa mabawa 16 ya majitaka na ukarabati wa mfumo wa majitaka.




Dk. George Dilunga wa Idara ya Magonjwa ya Dharura katika Hospitali ya Benjamini Mkapa akizungumza na watoto wanaoishi makao ya kitaifa ya kulelea watoto Kikombo, watumishi wa hospitali hiyo walipotembelea kituo hicho jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tume ya kuwachunguza mahakimu yaanzishwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Katibu Ajira na Uteuzi kutoka Tume ya Utumishi wa Mahakama nchini, Enziel Mtei, amesema Mahakama imeanzisha tume ya kuchunguza mahakimu mahakamani ili kuleta uwazi na kutenda haki mbele ya jamii.

Aliyasema hayo juzi wakati wa ufunguzi wa semina kwa waandishi wa habari kuhusu majukumu ya Tume ya Utumishi wa Mahakama nchini.

Alisema zipo kamati nne ambazo hutumika kuwawajibisha mahakimu pale wanapokwenda kinyume na maadili ya kazi zao za kila siku za ujenzi wa taifa na utoaji haki kwa jamii.

Alisema ili kuleta uwazi Mahakama imeweka tume ya kuchunguza mahakimu na lengo kuu likiwa ni kufanya kazi kwa kutenda haki mbele ya jamii na taifa kwa ujumla.

Aidha, aliwataka waandishi wa habari kueleza matatizo wanayokutana nayo ili ziweze kuwasilishwa na kufanyiwa kazi na tume hiyo kwa ajili ya manufaa ya taifa.

"Tume hii inatarajia kuandaa mafunzo mengine baada ya haya ya awali kwa wanahabari, lengo ikiwa ni kuwajengea uwezo waandishi wa habari ili waweze kuuhabarisha umma habari sahihi kuhusu tume hii," alisema.

Kadhalika, aliwataka waandishi wa habari ambao wamepata mafunzo hayo kufanya kazi kwa ushirikiano na tume hiyo, ikiwamo kutambua majukumu yake.

Hata hivyo, alisema anaamini mafunzo hayo yatawasaidia wanahabari katika kazi zao ambazo wanazofanya pamoja na Tume ya Utumishi wa Mahakama hapa nchini.

Akielezea majukumu ya tume hiyo alisema yamegawanyika katika kada mbalimbali ambapo nyingine zipo chini ya Rais kwa upande wa utawala.

Alisisitiza pia suala la nidhamu kwa waandishi wa habari katika kazi zao za kila siku zinazohusu Mahakama, huku akiwataka kuzingatia maadili kwenye utendaji wao wa kila siku.

# 'Wakulima watumieni maofisa ugani kupata ushauri'

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

MKURUNGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, Dk. Omary Nkulo, amewataka wakulima kuwatumia maofisa ugani kupata ushauri kuhusu aina ya mazao wanayotakiwa kupandwa kwenye maeneo yao.

Aliyasema hayo jana wilayani hapa, wakati alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya msimu wa kilimo wakati huu ambapo mvua zimeanza kunyesha.

Alisema wakulima wilayani hapa wanatakiwa kuwatumia maofisa ugani katika kuwashauri aina ya mazao yanayotakiwa kupandwa kwenye maeneo yao ili kuwa na uhakika wa chakula.

Dk. Nkulo alisema kuna maofisa ugani wa kutosha kwenye halmashauri hiyo na wamepatiwa vifaa vya kupima udongo kwenye maeneo yao kabla ya kuwaruhusu wakulima kupanda mazao yao.

Aidha, aliwataka wakulima kuhakikisha wanawatumia kabla ya kupanda mazao yao ili kufikia malengo ya halmashauri hiyo katika kujitosheleza kwa chakula kwa msimu ujao wa mavuno.

Pia alisema hali ya chakula wilayani hapa ni nzuri na gunia moja la kilo 100 linauzwa kwa Sh. 60,000 hadi 65,000 sawa na Sh. 600 hadi 650 kwa kilo moja.

Dk. Nkulo alisema wakulima wa mahindi wameshaanza kupanda na wale wa mtama wanatarajiwa kupanda Januari mwakani.

Kadhalika alisema endapo mvua zikinyesha vizuri wanatarajia kupata mavuno mazuri ambayo yatasaidia kuongeza uchumi wa wananchi wa halmashauri hayo.

Pia alisema halmashauri hiyo ilipewa mbolea ya ruzuku tani 100 kwa awamu ya kwanza na wameagiza mbolea nyingine tani 500, hivyo wakulima wasiwe na wasiwasi kuhusu mbolea.

Alisema ghala kuu la mbolea kwa wilaya hiyo lipo eneo la Mbande kwa sababu ni rahisi kwa wakulima kulifikia kwa urahisi hasa wa Ukanda wa Kaskazini ambao ni wakulima wa mhindi.

Aliyataja maeneo hayo ambayo wanalima mahindi kwa wingi kuwa ni Mkoka, Songambele, Hembahemba, Kibaigwa, Mlali na Pandambili.

Aliyataja mazao makuu ya kilimo na chakula yanayolimwa kwenye halmashauri hiyo kuwa ni mtama, alizeti, ufuta, mahindi na viazi.

Dk. Nkulo alisema uhakika wa soko la mazao hayo lipo ila wakulima wanatakiwa kuanza na zao la chakula kabla ya kulima zao la biashara.





# Wanafunzi wapewa msaada vitabu kujiandaa na mitihani

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

VITABU zaidi ya 100 vya masomo mbalimbali vimetolewa na umoja wa wazawa wa Kyela waishio ndani na nje na nchi (Kyela Ibasa Festival) kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi wa sekondari kujiandaa na mitihani.

Mwenyekiti wa kamati jamii katika kundi hilo, Vanessa Nyesyenge alikabidhi vitabu hivyo jana kwa Diwani wa Kata ya Ikimba, Omary Rashid Mwinyijuma.

Vanessa alisema vitabu hivyo ambavyo vitakabidhiwa kwenye Shule ya Sekondari Njisi kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi kumaliza mada kwa wakati ili kupata muda wa kujisomea.

"Miongoni mwa maono ya Ibasa ni kuisaidia jamii ya Kyela katika nyanja ya elimu wakati tunaadhimisha miaka mitano tangu kuanzishwa kwa Ibasa tumetoa misaada ya madawati na sasa vitabu ambavyo tunaamini vitaongeza chachu ya wanafunzi kusoma kwa bidii maana vitabu vipo," alisema Vanessa.

Aliongeza kuwa vitabu 150 vya masomo ya hisabati, kiingereza, fizikia, kemia, Kiswahili, bailojia, jiografia na uraia.

Akipokea msaada huo kwa niaba ya serikali, Diwani wa Kata ya Njisi, Omary Mwinyijuma alisema vitabu hivyo vitasaidia kuongeza ufaulu kwa wanafunzi hao kwa sababu watajifunza vizuri kwa nadharia kwa sababu tayari watakuwa mwongozo.

Aliwataka wanafunzi wa Shule ya Sekondari Njisi kuvitumia vitabu hivyo kuongeza maarifa ili waweze kufanya vizuri kwenye mitihani yao.

Akizungumza kwa niaba wanachama wa Kyela Ibasa, Sady Mwang'onda, alisema umekuwa ni utaratibu kila unapofika mwisho wa mwaka wazawa wote wa Kyela wanahamasishana kurudi nyumbani kuisaidia jamii yao kwenye nyanja ya afya, elimu, kuenzi utamaduni na kutembelea vivutio vya utalii.

Naye Sara Mwangasa, alisema wataendelea kutoa misaada ya hali na mali kwa jamii yao na kwamba wanatamani kuona Wilaya ya Kyela inapiga hatua ya maendeleo.

Makamu Mwenyekiti wa Umoja huo, Farida Mwakalyelye, alisema katika kuisaidia jamii mwaka 2024 wametoa Sh. milioni 4.9 kusaidia masuala mbalimbali.

# UWT yapewa siri kuwa wajasiriamali, kujiinua kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu,** KYELA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Patrick Mwalunenge amewashauri Jumuiya ya Umoja wa Wanawake (UWT) mkoani hapa kuanzisha SACCOS ili waweze kujiinua kiuchumi.

Alitoa ushauri huo wilayani Kyela kwenye hafla ya kuwapongeza wanawake wa chama hicho kwa kuwa wajasiriamali wazuri na kuinua uchumi wa familia.

Hafla hiyo iliandaliwa na Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya ambaye ni Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi.

Alisema wanawake wa mkoa huo wamekuwa na mchango mkubwa katika kuchangia maendeleo ya familia kutokana na shughuli za kiuchumi wanazofanya.

Alisema ili uchumi wa wanawake hao uwe endelevu ni muhimu waunde SACCOS ambayo itawasaidia kukopeshana kwa masharti nafuu na kuachana na mikopo ambayo imekuwa ikiwaumiza.

"Nakupongeza mheshimiwa mbunge kwa kuwa na wazo la kuinuana kiuchumi kwa wanawake, lakini ili msonge mbele zaidi ni vema ukawasaidia wanawake hawa kuanzisha SACCOS ya UWT ambayo itakuwa msingi mkubwa wa wao kukopesheka na kuendesha shughuli zao," alisema Mwalunenge. Alisema atahakikisha anawaunga mkono wanawake hao kwenye wazo hilo kwa kuwaunganisha na taasisi za kibenki, huku akiwataka wabunge wengine wa mkoa huo kuiga mfano wa Mbunge Mahundi katika kuhakikisha wanawainua watu wao kiuchumi kwa kuwa chama hicho kinapenda kuona watu walioko kwenye jumuiya zake wanakuwa na uchumi mzuri. Wakiwa kwenye hafla hiyo, wanawake hao walipata nafasi ya kueleza shughuli wanazozifanya za kujiingizia kipato baada ya mbunge Mahundi kuwawezesha mtaji mwaka 2022.

Walimshukuru kwa jitihada anazozifanya kwao na kuongeza kuwa kwasasa wamejikwamua kiuchumi na wanategemewa kwenye familia zao.

Mmoja wa wanawake hao, Kissa Fungo anayejishughulisha na shughuli za ushonaji nguo alisema baada ya kuwezeshwa mtaji wa Sh. 50,000 aliongeza biashara nyingine ya kuuza juisi ambapo mpaka sasa amefikisha mtaji wa Sh. milioni 1.5.

Kwa upande wake Mbunge wa Viti Maalumu na Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi alisema moja ya ajenda ndani ya UWT ni kuhakikisha wanawake wanakuwa na uchumi mzuri.

Hivyo aliwataka wanawake kujishughulisha na shughuli za kiuchumi badala ya kuwategemea waume zao pekee ili kujenga familia zenye uchumi imara. Naye Mkuu wa Wilaya ya kyela, Josephine Manase, aliwaalika wawekezaji wa ndani na nje kwenda kuwekeza wilayani humo kwenye sekta mbalimbali.

Alisema zipo fursa nyingi za uwekezaji ikiwemo kilimo, uvuvi pamoja na maeneo ya kujenga hoteli kwenye mwambao wa Ziwa Nyasa.



Baadhi ya wakazi wa Kata ya Matanji katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wakichambua vitambulisho vya taifa kwenye Ofisi ya Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wakulima watakiwa kufuata kanuni, taratibu za kilimo

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKULIMA wa Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe, wametakiwa kufuata kanuni na taratibu bora za kilimo na kuachana na kulima kwa mazoea.

Wito huo umetolewa na Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Beatrice Tarimo, wakati akizungumza na wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ambao walipewa miche ya parachichi katika ofisi za Kata ya Kitisi.

"Msimu wa kilimo nashukuru wanamakambako ni wachapa kazi, tunakwenda kuhamasisha watu wapande mbegu bora, serikali imeweka ruzuku kwenye mbolea watumie mbolea za kupandia na kukuzia, pia tudhibiti wadudu na magonjwa kwenye mashamba yetu, alisema Tarimo.

Alisema kwa mujibu wa mamlaka za hali ya hewa mvua mwaka huu ni nyingi, hivyo aliwatoa hofu wakulima kwamba wanapaswa kulima kwa tija sambamba na kutumia mbegu za muda mrefu na za muda mfupi ili wapate mazao mengi.

"Nawaomba mtunze miche hii hasa katika kipindi hiki cha mvua kwa sababu msipoitunza kwa kuweka dawa itaharibiwa na wadudu," alisema Tarimo.

Naye Ofisa Maendeleo Jamii ambaye ni mwezeshaji wa (TASAF) Halmashauri ya Mji Makambako, Hassan Abdallah, aliwataka wanufaika kutumia vyema fedha wanazozipata na kuitunza miche hiyo ili kukuza kipato chao.

"Tunatoa elimu na kuwakumbusha matumizi sahihi ya hizi fedha na tunawafundisha na kuelekeza kwenye ile miradi ya maendeleo kwa sababu leo TASAF ipo kesho mpango unaweza ukasitishwa kwa hiyo wao wanacho kitu cha kujikwamua kwa kupata miche," alisema Abdallah.

Baadhi ya wanufaika wa mfuko huo, Kulwa Gadau, Omari Sanga na Jane Njogolo walisema watahakikisha wanaitunza miche hiyo na kueleza kuwa changamoto kwa baadhi yao ni kukosa maji ya uhakika na ardhi yao kukumbwa na mchwa.

Alisema; "Tutajitahidi kutunza halafu kama kuna tatizo lolote tutawafuta, changamoto kubwa kwenye parachichi ni wadudu, pamoja na kutolima zao lingine mule kwenye parachichi hususani mahindi kwa sababu yanawadudu ambao wanaenda moja kwa moja kushambulia parachichi".





# Watakiwa kutumia uchumi wa buluu kuimarisha uchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Uvuvi na Uchumi wa Buluu, Suleiman Masoud Makame, amewataka wanawake kuzitumia fursa za uchumi wa buluu kwa ajili ya kukuza na kuimarisha uchumi.

Amewataka kujielekeza katika ufugaji wa mazao ya baharini ya matango bahari, mwani pamoja na kaa ambayo yanaweza kubadilisha hali zao za maisha kubwa bora.

Alitoa wito huo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari visiwani hapa kuhusu mafanikio ya miaka mitatu ya uongozi wa Rais wa Zanzibar, Dk.Hussein Ali Mwinyi pamoja na maadhimishi ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema serikali imekuja na sera ya uchumi wa buluu kwa ajili ya kuwashirikisha wananchi ikiwamo wanawake katika juhudi za kukuza uchumi.

Alisema Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu imetenga Sh. bilioni 36 kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kuingia katika uvuvi wa mazao ya baharini ikiwamo ujenzi wa mabwawa 100 kwa ajili ya ufugaji wa samaki na matango bahari.

Aidha alisema uvuvi wa buluu na mazao ya baharini ni sehemu ya maono ya Rais wa Zanzibar Dk. Mwinyi kuelekea uchumi wa buluu ambao lengo lake kuona wananchi wananufaika na rasilimali za baharini.

Waziri huyo alisema katika kipindi cha miaka mitatu mabwawa 100 yamejengwa kwa ajili ya ufugaji wa mazao ya baharini ikiwamo matango bahari pamoja, samaki na kaa.

Makame alisema Sh.bilioni 1.7 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa hayo ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kuwawezesha wananchi.

# Makamu wa Rais ahimiza upandaji miti, utunzaji uoto

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema ili kuendelea kuwapo rasilimali ya maji ardhini visiwani Zanzibar ni lazima hatua zichukuliwe la uhifadhi wa mazingira, kupanda miti na kutunza uoto wa asili ulipo.

Alitoa wito huo jana Masingini Wilaya ya Magharib 'A' Unguja wakati akifungua mradi wa uimarishaji na uhuishaji wa mfumo wa usamabazaji maji visiwani Zanzibar, ikiwa ni maandalizi ya kuelekea maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema kwamba kwa kufanya hivyo ndio njia pekee ya kuiendeleza rasilimali hiyo iendelee kuwapo na kuwanufaisha Wazanzibari. Alisema kwamba ni jukumu la kila mwananchi na viongozi kuutunza mradi huo kimazingira na kimiundombinu ili kuhakikisha kwamba mradi huo ni wa watu wote kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Othman alisema katika kutilia mkazo suala la utunzaji wa mazingira serikali kupitia ofisi yake itazindua mradi mkubwa wa upandaji miti Unguja na Pemba, jambo litakalohitaji ushiriki wa kila mwananchi na viongozi.

Pia aliwataka wananchi kuhakikisha wanalipa bili za maji ili kuifanya miradi ya maji kuwa endelevu na kuendelea kuwanufaisha wananchi wa Zanzibar.

Aidha, alisema kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imelipa umuhimu mkubwa suala la maji kwa kufanya juhudi za kuhakikisha ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya aina mbalimbali.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Joseph John Kilangi, aliwatahadharisha wananchi watakaofungiwa mita za maji kuhakikisha hawazichezei.

Alisema wananchi milioni 1.5 wataunganishwa kwenye mfumo wa kisasa wa mita za kisasa na kuwataka wananchi wote kuendelea kuitunza miundombinu hiyo sambamba na kuwa na subira wakati serikali ikiendelea na mipango ya kukamilisha malipo.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa ZAWA, Dk. Salha Mohammed Kassim, alisema mradi huo umegharimu Dola za Marekani milioni 92.18 na utekelezaji wa mradi umenza Aprili mwaka 2020 ambao umegawanyika katika sehemu tatu za utekelezaji.

Aidha, alisema kwamba skimu ya Masingini imejumuisha uchimbaji wa visima vinane vikubwa ambavyo vimekamilika na vinauwezo wa kuzalisha lita 890,000 kwa saa, utawanufaisha wananchi wa Masingini, Mtufaani, Mwera na Mwembe Mchomeke, ambapo kazi ya ulazaji wa mabomba imekamilika.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Aboud Jumbe, akizungumza na wafanyakazi wa Kampuni ya The Guardian Ltd ofisini kwake Maisara Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali: Huduma za afya zitatolewa bila ubaguzi

**Na Mmwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema inaendelea kuimarisha huduma za afya mijini na vijijini ili kuwapatia huduma bora za kijamii wananchi bila ya ubaguzi.

Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla aliyasema hayo jana wakati akifungua Kituo cha Afya cha Uzi na Ng'ambwa Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema kuwa ili nchi iwe na uchumi imara na maendeleo endelevu ni lazima wananchi wake wawe na afya bora itakayowapa nguvu za kufanya shughuli zao ambazo zinawapatia kipato pamoja na kukuza uchumi wa nchi.

Hemed alisema Kituo cha Afya cha Uzi na Ng'ambwa kilichojengwa na fedha za Mradi wa TASAF kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kimekamilika na asilimia ndogo iliyobaki serikali itatoa fedha.

Hivyo alimuagiza Waziri wa Afya kuhakikisha madaktari watakaotoa huduma katika kituo hicho lazima waishi maeneo ya karibu na kituo ili kuwahudumia wagonjwa kwa saa 24.

Aidha, aliitaka Wizara ya Afya kuandaa utaratibu wa kutafuta vijana wenye taaluma ya afya kutoka maeneo ya Uzi na Ng'ambwa na kuwasaidia kuwasomesha kada za afya ili kuwaandaa kufanya kazi katika kituo hicho.

Pia aliwataka wananchi wa Uzi na Ng'ambwa kutoa ushirikiano kwa serikali pamoja na madaktari wanaotoa huduma katika kituo hicho na vituo vingine ili kutoa huduma zilizobora na kufikia malengo ya serikali ya kuwapatia huduma bora wananchi wake bila ya kujali tofauti za aina yoyote.

Naye Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema jengo la kituo hicho cha afya limekamilika na limekidhi viwango vyote, kitatoa huduma za matibabu ya aina mbalimbali zikiwamo za mama na mtoto.

Alisema wizara itahakikisha inalitunza jengo hilo ili kutoa huduma zilizo bora pamoja na kufikia lengo la serikali ya kutoa huduma bora kwa wananchi wote bila ya kujali itikadi zao, sambamba na kuwajengea nyumba za makazi madaktari watakaofanya kazi katika kituo hicho ili kuwarahisishia ufanyaji wa kazi zao.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Dk. Islam Seif Salum alisema ujenzi wa kituo hicho kimejengwa na TASAF kwa kushirikiana na Wizara ya Afya Zanzibar na Wananchi wa Uzi na Ng'ambwa ambacho kimegharimu zaidi ya Sh. milioni 360.

Alisema kuwa kituo hicho kitatoa huduma za matibabu ikiwamo ya uzazi, meno, mama na mtoto na huduma za maabara ambazo zitatolewa kwa saa 24 kwa wananchi wote.

# TAWA yatoa ufafanuzi mamba kupigwa risasi

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) imetoa ufafanuzi wa madai yanayotolewa dhidi yake kuhusu kuwapo kwa raia wa kigeni anayehusishwa na mauaji ya mamba aliyeonyeshwa kwenye mitandao ya kijamii.

Kupitia mtandao wa mtu binafsi iliandikwa maelezo yakiinyooshea kidole serikali dhidi ya dai la kuwapo kwa raia wa kigeni kuua mamba mkubwa akitegemea kuweka rekodi ya dunia.

Taarifa ya TAWA iliyotolewa juzi na Kitengo cha Uhusiano kwa Umma, ilifafanua kuwa, uwindaji wa kitalii hufanyika kwa mujibu wa sera na sheria za nchi na kuutaka umma kupuuza taarifa hiyo ambayo imeleta taharuki kwa jamii.

"TAWA inapenda kuufahamisha umma kuwa, uwindaji wa kitalii unafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya mwaka 2009 iliyofanyiwa marekebisho 2022, pamoja na kanuni zake za uwindaji wa kitalii za mwaka 2015, zilizofanyiwa marekebisho mwaka 2017, 2019 na 2020," ilisema taarifa.

Kadhalika taarifa hiyo ilisema uwindaji wa kitalii pia, husimamiwa na Mkataba wa Kimataifa wa Biashara ya Wanyamapori na Mimea iliyo hatarini kutoweka.

"Mamba ni miongoni mwa wanyamapori wanaowindwa na mkataba huu na wamewekwa katika kundi la pili ambalo linaruhusu matumizi ya uvunaji ikiwamo uwindaji wa kitalii," ilisema.

Katika taarifa hiyo, TAWA imetaja masharti ya uwindaji wa mamba kuwa ni pamoja na kuhakikisha wote wanaowindwa nchini hawazidi idadi ya 1,600 kwa mwaka.

Masharti mengine yaliyotajwa kwenye taarifa hiyo ni kuhakikisha mamba anayewindwa ana urefu usiopungua sentimita 300.

"Masharti mengine ni ngozi za mamba wanaowindwa hufungwa vibandiko maalum na nyara zitokanazo na waliowindwa husafirishwa kwa vibali vya CITIES (CITES Esport Permit).

"Kuhusu video iliyosambaa, kumbukumbu tulizonazo ni kuwa TAWA ilitoa kibali Na. P 0001869 kuwinda mamba katika kitalu cha Ziwa Rukwa GP Agosti 28, 2023," ilisema.

Taarifa hiyo ilitaja faida zinazopatikana kwa uwindaji huo kuwa ni pamoja na malipo ya ada ya kitalu cha uwindaji wa kitalii cha Ziwa Rukwa ambao ulifanyika kwa Dola 185,000.

Taarifa hiyo ilisema ada ya leseni ya mwindaji bingwa aliyesimamia na kumwongoza mgeni ni Dola 2,000, malipo ya kibali cha uwindaji ni Dola 1,700.

"Ajira kwa watumishi wa kampuni wanaokuwapo kambini pindi mgeni anapowasili, mapato mengine kutokana na matumizi ya mgeni ikiwamo ununuzi wa chakula, vinywaji, usafiri wa ndege, visa (hati ya kusafiria) na magari yaliyotumika kumsafirisha.

"Uwindaji unasaidia kupunguza tatizo la wanyamapori wakali ambao utafiti unaonyesha wanyamapori wengi waliozeeka hushindwa kuwinda, hivyo hutoka katika mazingira ya asili na kuwa mgogoro kwa wananchi," ilifafanua taarifa hiyo.



Mkuu wa Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, Lazaro Twange, akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Sangara, Kata ya Riroda kuhusu utunzaji wa mazingira na kutoharibu misitu juzi. **PICHA: GIFT THADE**

# Mahakama Kuu yapokea nyaraka kesi mgogoro wa shule

**Na Jenesta Jasson, MULEBA**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania, Kanda ya Bukoba mkoani Kagera, imeendelea kusikiliza kesi ya mgogoro wa Shule ya Jipemoyo, Kata ya Ngenge wilayani Muleba, mkoani Kagera kwa kupokea nyaraka za umiliki kutoka pande zote mbili.

Shauri hilo lilifikishwa mahakamani hapo kwaajili ya kuweka zuio kwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Muleba kukabidhi shule hiyo inayomilikiwa na Mmisionari wa Kanisa Katoliki, Dk. Gozibert Byamungu kwa Haruna Mfunda, anayedai kuinunua kutoka kwa mdogo wa mmiliki huyo aliyetajwa kwa jina la Mukurasi ambaye kwa sasa ni marehemu.

Jana, mahakama hiyo chini ya Jaji Ayoub Mwenda, ilipokea nyaraka za umiliki kutoka kwa mlalamikiwa Haruna Mfunda, zilizomtaja kuwa mmiliki halali.

Upande wa mlalamikaji, Dk. Gozibert Byamungu, kupitia Wakili wake Prosper Mulokozi uliwasilisha pia mahakamani hapo nyaraka walizodai ni za umiliki halali wa shule hiyo.

Baada ya Mahakama kupokea nyaraka kutoka pande zote mbili iliahirisha shauri hilo mpaka Januari 14, 2024 baada ya mahakama hiyo kupata nyaraka kutoka kwa Kamishna wa Elimu zinazothibitisha umiliki halali wa shule hiyo ili watolee uamuzi.

## Chalamila, Muliro wakoleza moto vita dawa za kulevya

**Na Halfani Chusi**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, amesema kukamata watu wanaojihusisha na dawa za kulevya, ni operesheni endelevu katika mkoa huo kwa kuwa ndio lango kuu kiuchumi, kidiplomasia na kibiashara.

Chalamila alitoa kauli hiyo jana jijini alipofuatana na Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Murilo, walipokwenda kuipongeza Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) kwa kukamata kiwango kikubwa zaidi cha dawa za kulevya, zaidi ya tani tatu hivi karibuni.

Alisema dawa hizo zingesambazwa ndani na nje ya nchi, athari yake ingekuwa kubwa zaidi kwa taifa la kesho.

Alikumbusha kuwa siku chache zilizopita, walikamata baadhi ya viwanda vilivyokuwa vinatengeneza biskuti zilizochanganywa na dawa za kulevya.

"Nimeongea na Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo, ameniambia hakuna atakayeonewa na kila atakayekamatwa, watahakikisha kuna ushahidi wa kuhusika kwa kuuza, kusambaza au kununua," alisema Chalamila.

Mkuu wa Mkoa alisema wamebaini dawa hizo zinauzwa mitaani na vijiweni. Jeshi la Polisi limejipanga kwenye eneo hilo kuhakikisha wanatokomeza.

"Sisi katika Mkoa wa Dar es Saalam tumeendelea kuteua na kuunda vikosi kazi mbalimbali kutokomeza dawa za kulevya na kudhibiti wakwepakodi na wanaoingiza bidhaa kwa magendo kutoka mataifa mengine.

"Kwa mfano, wanaotumia njia ya Mbweni, Kunduchi, Pemba Mnazi Kigamboni, maeneo hayo kuna operesheni maalum imeshaanza na itakuwa na matokeo chanya," alisema.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro alisema mara nyingi wahalifu wanaokutwa na makosa ya kijinai, nusu au robo tatu yao huwa wametumia dawa za kulevya kwa kuwa wanaamini wakitumia wanapata ujasiri.

Alitoa angalizo kuwa watu hao wanaondoa ubinadamu, wanaweza wakapora watu, kukata mapanga, kubaka na kufanya matukio makubwa ya ukatili.

Kamanda Muliro alisema vita dhidi ya dawa za kulevya ni kubwa. Jeshi la Polisi, lazima liunge mkono kwa nguvu kile kinachofanywa na DCEA.

"Jiji litaendelea kuwa salama leo, kesho na keshokutwa. Tunajitambua, masuala ya rushwa tumewaambia yeyote atakayetusaliti hatutamwacha salama. Kama mifumo ya kijeshi inavyoeleza 'msaliti tutamshughulikia kuliko hata mhalifu'," Kamanda Muliro alionya.

Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo, alishukuru viongozi hao kwa kupongeza utendaji wa mamlaka hiyo, akisisitiza e kufanya kazi kwa uzalendo.

Alisema wataendelea kufanya operesheni kwa nguvu zote, akiwataka watumiaji na wauzaji wa dawa za kulevya kuacha mara moja. Huu si wakati wa kufanya biashara hiyo nchini.

"Tutafanya kazi kwa uzalendo mkubwa, tutaifanya kwa umakini na kila anayefanya atachukuliwa hatua. Wanasiasa, wazazi, viongozi wa dini tushirikiane pamoja kukemea," alisema.

## MATOKEO DRC:

# Rais Tshisekedi ang'ara kwa 77%, jeshi lazima maandamano mitaani

**KINSHASA, DRC**

ZOEZI la kuhesabu kura na kutoa matokeo linaendelea nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), huku Rais, Felix Tshisekedi akiwa anaongoza na kuwaacha kwa mbali wapinzani wake.

Hata hivyo, maandamano yaliyopangwa kuanza jana na vyama vya ushindani yalizimwa na vikosi vya ulinzi na usalama vya nchi hiyo.

Wagombea wa upinzani wameyakataa matokeo hayo kwa madai kuwa uchaguzi uliendeshwa katika hali ya udanganyifu na kushinikiza urudiwe.

Hadi usiku wa kuamkia jana, Tume ya Uchaguzi (CENI), ilitangaza matokeo ya kura zaidi ya milioni 9 ambazo zimehesabiwa . Rais Felix Tshisekedi anayewania muhula wa pili anaongoza kwa kupata kura milioni saba sawa na asilimia 77, akifuatiwa na mpinzani wake wa karibu Moise Katumbi akiwa na asilimia 15.

Anayeshika nafasi ya tatu Martin Fayulu amejikusanyia asilimia 4 ya kura zote.

Katika matokeo hayo, Rais Tshisekedi anaongoza kwa idadi kubwa ya kura katika majimbo 21 kati ya 26 pamoja na jiji kuu la Kinshasa.

Katumbi yeye anaongoza katika majimbo manne ya kusini mashariki ya Haut-Katanga, Tanganyika, Lualaba na Haut-Lomami.

Matokeo ya jumla ya uchaguzi wa Rais yanatarajiwa kutangazwa jumapili ya Desemba 31.

Hata hivyo, kambi ya upinzani imepinga matokeo hayo ya awali na kusema yalipangwa na tume hiyo ili kumpa ushindi Rais Tshisekedi.

Olivier Kamitatu ambaye ni msemaji wa Moise Katumbi alisema uchaguzi lazima urudiwe na hawana muda wa kupeleka malalamiko yao katika mahakama ya katiba. "Vyombo vyote vinavyosimamia mchakato wa uchaguzi vinaongozwa na wanachama wanaohusishwa na Felix Tshisekedi. Kwa hiyo, Mahakama ya Katiba itaendeleza tu udanganyifu ambao tayari umepangwa.", alisema Kamitatu.

Alisema kuwasilisha malalamiko kwenye mahakama hiyo ni sawa na kuhalalisha ulaghai wa mwenyekiti wa tume hiyo ya uchaguzi Denis Kadima.

Aidha, msemaji wa serikali, Patrick Muyaya, alikosoa kauli hiyo kwa kueleza vyama vya upinzani vinapanga kuandaa vurugu.

Muyaya aliambia shirika la habari la Ujerumani (DW) kwamba hawatakubali machafuko kutokea na kuitaka kambi ya upinzani kusubiri hadi matokeo kamili ya uchaguzi yatakapotangazwa.

Katika hatua nyingine, jeshi la polisi lilitumia mabomu ya machozi kuwatawanya waandamanaji katika wilaya ya Kasavubu. Mgombea wa urais Martin Fayulu, ambaye ni mmoja wa watu walioitisha maandamano amelaumu polisi kwa kutumia nguvu kuwatawanya waandamani na kusababisha watu 11 kujeruhiwa kwa kupigwa risasi.

Aidha, waangalizi wa uchaguzi kutoka Kanisa la Katoliki na la kiprotestanti nchini humo wanatarajiwa kutoa ripoti yao jana jioni kuhusu uchaguzi huo.

**DW**



Polisi wa DRC wakipambana kuzima moto uliowashwa na waandamanaji wanaopinga matokeo ya uchaguzi yanayoendelea kutangazwa nchini humo. **PICHA: AFP**

# Mazungumzo ya meza moja ya majenerali yaahirishwa

**KHARTOUM, Sudan**

MAZUNGUMZO ya ana kwa ana kati ya viongozi wa makundi yanayopigana nchini Sudan yaliyopangwa kufanyika jana nchini Djibout yameahirishwa.

Katika taarifa iliyotolewa jana ilieleza mkutano huo kati ya wababe wa kivita Jenerali Fattah Al Burhan wa jeshi la nchi hiyo na Jenerali Mohamed Hamadn Dagalo, mkuu wa kikosi cha Rapid Support Forces (RSF), utafanyika mwezi unaokuja.

Hata hivyo, tarehe kamili ya kufanyika kwa mazungumzo hayo bado haijajulikana.

Mkutano huo ungekuwa wa kwanza kati ya viongozi hao wawili wanaovutana kuhusu uongozi na kusababisha kuibuka kwa mapigano tangu mwezi wa Aprili.

Katika mapigano hayo, maelfu ya watu wameuawa na wengine zaidi ya milioni saba wamekimbia makazi yao.

Mgogoro huo umetajwa kuwa ni mbaya zaidi na Umoja wa Mataifa ambao umesababisha watu kuhama makazi.

Wakati huo huo, mapigano yameripotiwa kuendelea katika mji mkuu Khartoum.

Jenerali Dagalo alifanya ziara nchini Uganda na kukutana na kiongozi wa nchi hiyo Rais Yoweri Museveni na baadaye kuelekea Ethiopia kwa ajili ya kukutana na naibu waziri mkuu.

**BBC**

# Israel yaonya mapigano kuelekezwa hadi Lebanon

**TEL AVIV, Israel**

HUENDA vita vinavyoendelea kati ya jeshi la Israel na wanamgambo wa Hamas, vitapanuka na kuhusisha nchi jirani baada ya nchi ya Lebanon kutishiwa kushambuliwa.

Waziri asiye na Wizara Maalum, Benny Gantz, alionya nchi yake itachukua hatua ya kuiondoa Hezbollah kwenye mpaka na Lebanoni iwapo mashambulizi dhidi ya taifa hilo yataendelea.

Gantz alisema jeshi la nchi hiyo litaingilia kati ikiwa dunia na serikali ya Lebanon haitawazuia wanamgambo hao kufyatua risasi kaskazini mwa Israel.

Alisema wakati wa suluhu ya kidiplomasia ulikuwa ukiisha, na kwamba jeshi litachukua hatua.

Majibizano makali ya risasi yamekuwa yakiongezeka tangu Hamas iliposhambulia Israel Oktoba 7, katika eneo la mpaka kati ya Israel na Lebanon.

Hali hiyo imesababisha wasiwasi kwamba mzozo huo unaweza kusambaa katika eneo lote la Mashariki ya Kati.

"Hali kwenye mpaka wa kaskazini wa Israel inadai mabadiliko," alisema Gantz wakati akiongea na waandishi wa habari juzi.

Alisisitiza kwamba kama dunia na serikali ya Lebanon haitachukua hatua ili kuzuia wanamgambo hao kufyatulia risasi kwa wakati wa kaskazini mwa Israel, na kuwaweka mbali na mpaka, jeshi litafanya hivyo."

Waziri Gantz, ambaye ni mwanasiasa wa upinzani na kiongozi wa zamani wa jeshi la Israel, alijiunga na baraza la mawaziri la vita la Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu kama waziri asiye na wizara maalum.

# Korea Kaskazini yajiandaa kwa vita

**PYONG YANG, Korea Kaskazini**

RAIS wa Korea Kaskazini, Kim Jong Un, ameamuru jeshi la nchi yake, kitengo cha zana za kivita na silaha za nyuklia kuharakisha maandalizi ya vita ili kukabiliana na kile alichokitaja kuwa mapigano ambayo hajawahi kushuhudiwa na nchi ya Marekani.

Kiongozi huyo alisema hayo jana wakati akizungumzia mwelekeo wa kisera kwa mwaka mpya katika mkutano wa chama tawala.

Rais Jong Un aliongeza kwamba nchi yake itaongeza ushirikiano wa kimkakati na mataifa yanayopinga ubeberu.

Korea Kaskazini imekuwa ikiimarisha uhusiano wake na Russia na mataifa mengine huku Marekani ikishutumu nchi hizo mbili zinafanya biashara ya kuuziana silaha kwa ajili ya kuimarisha vita nchini Ukraine.

Katika hatua nyingine Rais wa Korea Kusini Yoon Suk Yeol jana alitembelea vikosi vya jeshi lake katika upande wa mashariki mwa nchi hiyo.

Katika ziara hiyo Rais Suk Yeol alikagua maendeleo ya ulinzi na kuapa kutoa majibu ya haraka ikiwa kutatokea uchochezi wa aina yoyote kutoka kwa Korea Kaskazini.

# KOCHA MAXIME ATUA IHEFU

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Ihefu FC jana umemtambulisha rasmi aliyekuwa Kocha wa Kagera Sugar, Mecky Maxime kuwa kocha wa timu hiyo.

Mecky ametambulishwa rasmi kupokea mikoba ya aliyekuwa kocha wa timu hiyo Mganda Mosses Basena aliyefungishiwa virango vyake baada ya uongozi kutoridhishwa na matokeo ya timu yao.

Akizungumza na Nipashe jana, Mtendaji Mkuu wa timu hiyo, Zagalu Chalamila alisema Mecky ni kocha mkubwa ndani ya Tanzania na mzoefu kisoka kwa ngazi ya klabu na timu ya Taifa.

Alisema uongozi wa timu hiyo unaimani kubwa na kocha huyo kuwafikisha sehemu sahihi katika mashindano mbalimbali ikiwamo michezo yao ya Ligi Kuu mzunguko wa pili.

"Kuanzia sasa kikosi cha timu yetu katika mashindano yote yaliyopo mbele yetu kitakuwa chini ya Mecky, hatukufanya vizuri mzunguko wa kwanza lakini tunaimani duru la pili tutafanya vizuri," alisema Chalamila.

Aliongeza kuwa wanafahamu ubora wa kocha huyo na suala la usajili wa dirisha dogo wamelikabidhi kwake kwa sababu ameiona timu hiyo na kuona mapungufu ya kikosi chake.

Chalamila alisema wamejipanga vizuri katika masuala ya usajili na wako kwenye mchakato wa kuimarisha timu yao kwa kushirikiana na kocha wao Mecky.




Meneja Huduma za Ziada wa Tigo, Adam Francis (kulia), akimkabidhi mpira jana mtaalamu wa huduma za ziada wa kampuni hiyo, Noreen Kira, ikiwa ishara ya kuzindua kampeni ya Soka la Afrika Limeitika inayolenga kuwapeleka wateja wake kushuhudia fainali za Afcon. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# NMB yatoa milioni 200/- Mapinduzi Cup

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imetoa zaidi ya shilingi milioni 200 kwa ajili ya zawadi za mashindano ya Kombe la Mapinduzi Zanzibar pamoja na traki suti 150 kwa ajili ya kuvaa kwenye matembezi Siku ya Mapinduzi.

Fedha hizo zimetolewa kwa ajili ya zawadi kwa bingwa wa michauno hiyo ambapo atazawadiwa shilingi milioni 100 na medali, mshindi wa pili atapata Shilingi milioni 70 na medali huku fedha nyingine ikitumika kwenye uwendeshaji wa mashindano hayo.

Akizungumza juzi wakati wa halfa ya kukabidhi nguo za mazoezi kwa ajili ya siku ya mazoezi kitaifa itakayofanyika Januari Mosi, Meneja Biashara wa Benki hiyo Zanzibar, Naima Said Shaame, alisema udhamini huo unalenga azma ya benki ya NMB na pia juhudi za serikali katika kusherehekea miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema benki hiyo ni miongoni wa wadau wakubwa wanaochangia ukuaji wa sekta mbalimbali za maendeleo Zanzibar waliona kuna umuhimu kuwa sehemu ya maadhimisho ya Mapinduzi ambayo kilele chake ni Januari 12.

"Kama benki tunasema huu sio mwisho wa udhamini wetu. Tunaamini kwamba michezo sio tu inachangia ustawi wetu, lakini pia inatuleta pamoja kama taifa," aliongeza.

Alisema NMB imeamua kutoa traki suti hizo za mazoezi 150 kwa ajili ya kuunga mkono siku ya mazoezi kitaifa jambo ambalo hulifanyika kila mwaka kuonyesha kuwa mazoezi ni muhimu kwa wananchi ambao ni wateja wao.

"Tunapenda kuwa na wateja wenye afya na tunajua kuwa mazoezi ni afya, hivyo tumeamua kuunga mkono jambo hilo ili kuhakikisha wateja wetu wanakuwa na afya njema," alisema.

Akizungumza baada ya kupokea traki suti hizo Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Fatma Hamad Rajab, aliishukuru benki hiyo kwa misaada mbalimbali inayotoa na kueleza kuwa benki hiyo ni kiongozi wa kutoa misaada kwa serikali katika nyanja zote za michezo na jamii.

## Balama, Makame kutua Mashujaa FC

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kukamilisha usajili wa mshambuliaji Emmanuel Mtumbuka kutoka Stand United kwa ajili ya kuongeza nguvu upande wa ushambuliaji, klabu ya Mashujaa FC iko kwenye hatua ya mwisho ya kuwasajili wachezaji Mapinduzi Balama na Abdul Makame Bui.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa viongozi wapo kwenye mazungumzo ya mwisho kuwasajili wachezaji hao kwa mkataba wa miezi sita kwanza ili kuangalia viwango na ufanisi wao wa kazi, kabla ya kuwaongeza miaka miwili kama watafanya vyema.

Balama anayecheza nafasi ya kiungo mshambuliaji na Bui ambaye ni kiungo mkabaji, wote wawili wameshawahi kuitumikia klabu ya Yanga.

Balama ni mmoja wa wachezaji walioachana na Coastal Union kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

Msemaji wa Klabu hiyo, Hamisi Milyango alithibitisha kuwa kwenye mazungumzo na wachezaji hao huku wakikamilisha usajili Mtumbuka.

"Tumemsajili mwamba, straika wa boli, Mtumbuka kutoka Stand United, jamaa anafunga mabao na kutengeneza 'assist' kweli kweli.

## Tigo kupeleka watu fainali za Afcon

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tigo imezindua kampeni maalum ya 'Soka la Afrika Limeitika' yenye lengo la kuwapa fursa wateja wake kwenda kushuhudia fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) zitakazofanyika Januari mwakani nchini Ivory Coast.

Fainali hizo za Afrika zimepangwa kuanza Januari 13 na kumalizika Februari 11 huku Tanzania ikishiriki kwa mara ya tatu fainali hizo.

Akizungumzam jana jijini Dar es Salaam, Meneja wa Huduma ya ongezeko la thamani wa kampuni hiyo, Adam Francis, alisema wateja wa kampuni hiyo wanaweza kujishindia zawadi mbalimbali ikiwamo safari ya kwenda Ivory Coast kushuhudia fainali hizo.

"Tunafuraha kuzindua promosheni ya 'Soka la Afrika Limeitika', inayowapa wateja wetu wapendwa fursa ya kipekee ya kuwa sehemu ya Kombe la Mataifa ya Afrika 2024. Promosheni hii sio tu inaendana na dhamira yetu ya kutoa uzoefu usio na kifani bali pia inasherehekea ushiriki wa Tanzania katika fainali hizi kubwa Afrika," alisema Francis.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**PHILLIPS NA NEWCASTLE**

KLABU ya Newcastle United ina imani kuwa inaweza kukubaliana kuhusu mpango wa kumsajili kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips kutoka Manchester City lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Juventus, Everton na Crystal Palace kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. **(Telegraph)**

**RATCLIFFE KULIPWA**

FAMILIA ya Glazer italazimika kumlipa Sir Jim Ratcliffe hadi pauni milioni 66 ikiwa watasitisha mpango wa kampuni yake ya Ineos Group kununua asilimia 25 ya hisa pale Manchester United. **(Independent)**

**MAN UNITED NA USAJILI**

PIA katika sehemu ya mpango huo, Ineos pia inabidi itoe ushauri kuhusu uhamisho wowote wa Manchester United katika dirisha la uhamisho la Januari na kocha Erik ten Hag hawezi kufukuzwa kazi bila kuhusika kwa Jim Ratcliffe. **(Standard)**

**NEVES MKATABA MPYA**

KIUNGO wa kati wa Ureno, Joao Neves mwenye umri wa miaka 19 ambaye amekuwa akihusishwa na kuhamia Manchester United, yuko kwenye mazungumzo kuhusu mkataba mpya katika klabu ya Benfica ambayo huenda ikaongeza kifungu chake cha kuachiliwa kutoka euro milioni 120 hadi euro milioni 130.**(O Jogo)**

**GYKERES AHUSISHWA**

MANCHESTER United inahusishwa na mshambuliaji wa Sweden, Viktor Gyokeres mwenye umri wa miaka 25 kutoka kwa wapinzani wa Benfica, Sporting Lisbon. **(Correio da Manha)**

**ARSENAL KUONGEZA WACHEZAJI**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema klabu hiyo iko tayari kuimarisha kikosi chake Januari „kwa sababu tunataka kuwa na nguvu zaidi“. **(Guardian)**

**DE LIGT ATAKIWA ARSENAL**

ARSENAL inavutiwa na mlinzi wa kati wa Bayern, Munich Matthijs de Ligt huenda kuna uwezekano wa kumnunua Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 24 Januari. **(Athletic)**

**ROBINSON AWANIWA**

LIVERPOOL imewauliza Fulham kuhusu kupatikana kwa mchezaji wa kimataifa wa Marekani, Antonee Robinson mwenye umri wa miaka 26, huku wakitafuta kusajili mlinzi wa kushoto katika dirisha la uhamisho la Januari. **(90min)**

**NYOTA KUONDOKA JANUARI**

KLABU ya Tottenham Hotspur imemwambia mlinzi wa England, Eric Dier mwenye umri wa miaka 29, kiungo wa kati wa Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg mwenye miaka 28 na mlinda mlango Mfaransa Hugo Lloris 37, kwamba wanaweza kuondoka katika klabu hiyo Januari. **(Football Insider)**

**GRIEZMANN KWENDA MAREKANI**

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Ufaransa, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 32 amesema Atletico Madrid itakuwa klabu yake ya mwisho barani Ulaya na angependa kumalizia soka lake nchini Marekani. **(AS)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND KUREJEA JANUARI MWISHONI

Nyota huyo amekosa mechi sita za mwisho za timu yake na sasa Kocha Pep Guardiola anaamini...

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola alisema „anatumaini“ Erling Haaland anaweza kurejea uwanjani kabla ya mwisho wa Januari baada ya kusema mshambuliaji huyo wa Manchester City bado hayuko sawa kufanya mazoezi na wachezaji wenzake.

Haaland mwenye umri wa miaka 23 sasa amekosa mechi sita za mwisho za City katika mashindano yote baada ya kushinda 3-1 kwenye Ligi Kuu Jumatano dhidi ya Everton.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway alipigwa picha na akaunti za mitandao ya kijamii ya klabu hiyo akipiga mpira wakati wa safari ya wiki moja ya City kwenda Saudi Arabia kwenye Kombe la Klabu Bingwa ya Dunia wiki iliyopita, lakini hajakaribia kurejea kikosi cha kwanza.

„(Haaland) anafanya mazoezi peke yake, hafanyi mazoezi na timu,“ alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari baada ya ushindi huo kwenye uwanja wa Goodison Park.

„Kevin (De Bruyne) amefanya mazoezi na timu, lakini Erling bado. Ni swali la lini maumivu yatatoweka.

„Tunatumaini atarejea Januari, lakini kuumia kwenye mfupa ni hatari sana. Yeye si kama Phil Foden mwenye ngozi ndogo -- Erling ni mkubwa.

„Atarejea na kucheza. Lakini ni juu ya madaktari. Madaktari wanakuja kila asubuhi na kusema mchezaji huyu anapatikana na huyu hayupo.“

Nahodha wa City, De Bruyne hajacheza tangu alipopata jeraha baya la misuli ya paja dhidi ya Burnley katika mchezo wa ufunguzi wa msimu huu, lakini Guardiola alisema kiungo huyo wa Ubelgiji anakaribia kurejea uwanjani na anaweza kuwa fiti kwa ajili ya mechi ya raundi ya tatu ya Kombe la FA dhidi ya Huddersfield Town Januari 6, 2024.

„Ndio yuko karibu,“ alisema Guardiola.

„Ningependa yeye kucheza mchezo unaofuata au dhidi ya Huddersfield, lakini ni muhimu kujiweka sawa kwa muda mrefu.“

City walipata jeraha lingine katika ushindi wa Everton huku beki John Stones akilazimika kutolewa nje katika kipindi cha kwanza kutokana na tatizo la kifundo cha mguu jeraha ambalo Guardiola alisema ni mapema mno kutathmini kiwango kamili alichoumia.

Kikosi cha Guardiola sasa kiko nyuma kwa pointi tano na vinara Liverpool wakiwa na mchezo mkononi, licha ya kushinda mara moja pekee katika mechi sita za ligi kabla ya safari ya Everton.

# MADUEKE: CHELSEA ILISTAHILI USHINDI



**LONDON, England**

NONI Madueke amesisitiza kuwa Chelsea ilistahili kuifunga Crystal Palace baada ya mkwaju wake wa penalti wa dakika za mwisho kupata ushindi wa 2-1.

The Blues walionekana kujiandaa kwa jioni nyingine ya kutatanisha huko Stamford Bridge baada ya kukosa nafasi nyingi kabla ya winga huyo kufunga mkwaju huo ikisalia dakika moja ya muda wa kawaida.

Bao la kusawazisha la Michael Olise lilifuta uongozi wa wenyeji katika kipindi cha kwanza ambao walikuwa wamepewa na Mykhailo Mudryk.

Akizungumza na Amazon Prime baada ya mchezo huo, Madueke alisema: "Ulikuwa mchezo mgumu.

"Sifa kwa Crystal Palace, walicheza vitu vizuri. Lakini sifa kwetu pia, tulistahili."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 aliingizwa uwanjani dakika ya 71 na kushinda mkwaju wa penalti baada ya kufanyiwa faulo na Eberechi Eze ndani ya eneo la hatari.

Palace walipiga mashuti matano yaliyolenga lango ikilinganishwa na manne ya Chelsea na kocha Eagles Roy Hodgson alihisi timu yake ilistahili zaidi kutoka kwenye mchezo huo.

# Spurs kusaka mlinzi mpya

**LONDON, England**

NYOTA wa Tottenham Hotspur, Cristian Romero hatacheza kwa angalau mwezi mmoja kutokana na jeraha la misuli ya paja na huenda klabu hiyo ya Ligi Kuu England ikahitaji kusajili beki mwingine wa kati, kwa mujibu wa kocha, Ange Postecoglou.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina, Romero alitoka wakati wa mapumziko wakati wa ushindi wao wa 2-1 nyumbani dhidi ya Everton Jumamosi iliyopita.

Spurs sasa hawana mabeki wao wawili bora wa kati huku Micky van de Ven akiwa nje ya uwanja tangu mapema Novemba na hatarajiwi kurejea hadi mwezi ujao.

"Hapana, hapana. Hafai. Amefanyiwa uchunguzi, hivyo atakuwa nje kwa wiki nne au tano," alisema Postecoglou kuhusu kutokuwepo kwa Romero kabla ya safari ya jana Alhamisi ya Ligi Kuu dhidi ya Brighton & Hove Albion.

"Kila mtu mwingine alipitia hilo sawa. Kuna miili michache yenye kidonda hapo lakini tumekuwa na, aina ya wiki ya mazoezi rahisi, siku chache zilizopita hata hivyo, lakini kila mtu yuko sawa."

James Maddison, Ivan Perisic, Ryan Sessegnon, Manor Solomon, Rodrigo Bentancur na Ashley Phillips ni wachezaji wengine waliokosekana kwa muda mrefu kwenye kikosi cha Spurs.

Postecoglou alisema mlinzi wa Uholanzi Van de Ven anaweza kurejea kwa ajili ya safari yao ya Manchester United Januari 14 na akakiri kuwa wanahitaji beki mwingine wa kati.

"Siweki hisa nyingi katika hali ya beki wa kati wa upande wa kushoto au kulia, tunahitaji tu mchezaji mwingine katika nafasi hiyo ambaye anaweza kutoa kina zaidi kwa ajili yetu na uwezo wa kuibadilisha," alisema.

# Arteta kuingia sokoni Januari

**LONDON, England**

MIKEL Arteta amesisitiza kuwa Arsenal iko tayari kuzama katika soko la usajili Januari ikiwa kikosi chake kitaendelea kuwa na majeruhi katika wiki za hivi karibuni.

Washika bunduki hao wapo katika wakati mzuri zaidi kuliko baadhi ya wapinzani wao wa Ligi Kuu kutokana na kuwa na majeruhi wachache, lakini jana Alhamisi waliwakosa wachezaji watano kwenye mechi dhidi ya West Ham.

Thomas Partey, Jurrien Timber, Fabio Vieira na Takehiro Tomiyasu wote bado hawajajumuishwa huku Kai Havertz alikosa mchezo huo kutokana na kadi tano za njano.

Arsenal iliwekeza zaidi ya pauni milioni 200 kununua wachezaji wapya katika msimu wa joto, ikiwa ni pamoja na usajili wa rekodi ya klabu wa Declan Rice kutoka West Ham kwa pauni milioni 105.

Kiungo huyo wa kati wa England aliunganishwa kwenye Uwanja wa Emirates na Havertz na Timber huku Arsenal ikitumia fedha nyingi baada ya kukosa ubingwa licha ya kuwa kileleni kwa siku 248 msimu uliopita.

Huku Arteta akiwa hana uhakika wa tarehe za kurejea kwa wachezaji wanne walio majeruhi, Mhispania huyo alithibitisha kuwa Arsenal wana mipango na uhitaji wa kusajili Januari.

Alisema: "Kwa sasa, ni vigumu sana. Tuna nafasi ambazo tumeziweka wazi sana kwa wiki sita zilizopita na tunatumaini tutawarudisha wachezaji. Katika hali gani na lini? Sijui.

"Hiyo ni alama ya kuuliza na vile vile kwa sababu tuna majeraha ya muda mrefu bado kwa wachezaji fulani ambayo yanatupa mabadiliko mengi.

"Tuna malengo Fulani, ikiwa mambo yatatokea. Vile vile, hatujui jinsi kikosi kitakavyokuwa katika muda wa wiki mbili na unapaswa kuwa tayari kila wakati kwa hilo.

"Lakini ni soko gumu sana ambalo linabadilika haraka sana na halitabiriki pia - na lazima uwe tayari," alisema Arteta

HABARI MICHEZO

# KMKM YAUPIGIA MAHESABU UBINGWA LIGI ZANZIBAR

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu ya Zanzibar KMKM wamesema bado katika malengo yao ya kutetea ubingwa wao msimu huu na kuweka historia ya kuchukua ubingwa huo mara nne mfululizo.

KMKM haikuanza vizuri ligi hiyo msimu huu ambapo kabla ya kumalizika mzunguko wa kwanza iliachana na kocha wake mkuu raia wa Burundi.

Timu hiyo mpaka sasa imecheza michezo 15 kwenye ligi na kufanikiwa kushinda michezo tisa, imetoka sare michezo miwili na kufungwa mechi nne, inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo kwa kuwa na pointi 29.

Akizungumza na Nipashe, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Ame Msimu alisema ingawa mzunguko wa kwanza hawakuwa bora hiyo haina maana kuwa watashindwa kutetea taji lao hilo.

Alisema timu hiyo katika mzunguko wa pili imeelekeza mipango yake ya kuhakikisha wananyakuwa taji la Zanzibar kwa mara ya nne mfululizo.

Alisema katika kufanikisha mpango huo timu hiyo itasajili wachezaji wapya wanne wote kutoka Visiwani Zanzibar ili kuziba nafasi ya wachezaji wanne ambao wanampango wa kuachana nao.

"Tunaenda katika mzungumo wa lala salama hivyo lazima tuhakikishe tunafanya maboresho makubwa ya kikosi, tutaimarisha timu kwa kuongeza wachezaji wengine, lengo letu ni kuhakikisha tunatwaa ubingwa," alisema Msimu.

Alisema wachezaji watakaowasajili wataongeza nguvu kwenye safu ya ushambuliaji, golikipa na beki mmoja wa kati.

Aidha alisema Ligi Kuu ya Zanzibar imekuwa ngumu kutokana na kila timu kujiandaa vizuri hivyo lazima wajiimarishe ili kuweza kutetea ubingwa wao.




Mwanariadha maarufu nchini India, Milind Soman (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusu mbio za kirafiki kati ya Tanzania na India zitakazofanyika kesho kuanzia Dar es Salaam hadi Bagamoyo, kushoto ni Makamu wa Rais wa Shirikisho la Riadha, William Kalaghe na Balozi wa India nchini, Biyana Predhan. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwanariadha India ahamasisha kujenga afya kupitia riadha

**Na Romana Mallya**

MWANARIADHA mashuhuri nchini India, Milind Soman, ameungana na Watanzania kuhamasisha afya na utimamu wa mwili kwa kushiriki mbio za marathoni zinazohusisha kutembea na kukimbia umbali mrefu.

Mbio hizo ambazo zinatarajia kufanyika kwa siku mbili kuanzia kesho, zitahusisha kilometa 130 ambapo washiriki wataanzia mkoani Dar es Salaam hadi Bagamoyo, mkoani Pwani.

Pia kwa wale wanaotaka kujenga afya zao si kushindana kutakuwa na mbio za kilometa tano na kilometa 10 ambazo zitaanza asubuhi.

Mbio hizo zimeandaliwa kwa ushirikiano wa Ubalozi wa India hapa nchini pamoja na Shirikisho la Riadha Tanzania (RT) zikiongozwa na mwanariadha huyo maarufu.

Akizungumza jana katika Ubalozi wa India nchini, Soman alitaka familia kuhamasishana kushiriki marathon hizo huku akitolea mfano wa familia yake kuwa, mama yake mwenye umri wa miaka 85, mke wake na watoto kuwa ni washiriki wazuri wa mbio.

Alisema mbio hizo moja ya lengo lake ni kuuweka mwili sawa na kuweza kupambana na magonjwa yakiwamo magonjwa yasiyoambukiza.

"Ninaamini watu watakuja na familia zao. Kwa hivyo, sio muhimu kwenda haraka. Unajua watu wengi hufikiri kwamba tukijiunga ni lazima tukimbie haraka," alielimisha.

Aliwakumbusha Watanzania kuwa ili kuondokana na magonjwa mbalimbali ni vyema watu kuhakikisha wanafanya mazoezi, wanalala kwa wakati, kula vyakula vya kujenga mwili pamoja na kuondokana na msongo wa mawazo.

Kwa upande wake, Balozi wa India nchini Tanzania, Pradhan Binaya, alisema ujio wa mwanariadha huyo mashuhuri ni matokeo ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan, hivi karibuni nchini India ambapo pamoja na mambo mengine, kulitiwa saini mikataba mbalimbali ikiwamo iliyohusu sekta ya michezo.

Alisema marathon hizo zitatanguliwa na warsha ya siku moja itakayofanyika leo katika Kituo cha Utamaduni wa India Swami Vivekananda (SVCC) kilichoko Masaki.

Katika hatua nyingine, Balozi Binaya, alitumia fursa hiyo kuwaaga Watanzania baada ya kubadilishwa kituo cha kazi kwenda New York, Marekani.

Alisema kuwa, ameona fursa nyingi, ametembea karibu mikoa yote Tanzania na kufungua maeneo ya ushirikiano ambayo ameeleza ni kazi iliyofanikiwa katika historia yake ya majukumu yake kidiplomasia.

Makamu wa Rais wa RT, William Kallage, alisema marathon za namna hii ni za kwanza kufanyika Tanzania hivyo, ameahidi zitakapofanyika mara kadhaa, shirikisho litazitambua.

"Ninaomba kusisitiza, tujisajili kushiriki mbio hizi ni bure. Haya ni mashirikiano kati ya Serikali ya India na Serikali ya Tanzania, hii ni ya kwanza na maelekezo ya serikali ni kwamba, mbio hizi zitakuwa za kudumu kwa kila mwaka," alisema.

## Pwani yatoa mshindi Twende Zetu Ivory Coast 2024 Ki-VIP

**Mwandishi Wetu**

MKAZI wa mkoani Pwani, Ally Kiseto ameibuka mshindi katika droo ya kampeni ya Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP.

Kampeni hiyo inayolenga kuwapeleka Ivory Coast watu sita kushuhudia mubashara fainali za mataifa ya Afrika (Afcon) inaendelea kote nchini kwa wiki ya tatu sasa ikiratibiwa na kampuni ya kubashiri ya Betika kwa kushirikiana na Tigopesa.

Droo kubwa ya kutangazwa washindi sita itafanyika Januari 2, na watakaopata tiketi hiyo watasafari kwa gharama za kampuni ya Betika kwenda Ivory Coast kushuhudia fainali hizo zitakazoanza Januari 13 hadi Februari 11.

Washindi hao wataishuhudia mubashara pia timu ya Tanzania (Taifa Stars) ambayo kwenye fainali hizo itacheza mechi yake ya kwanza Januari 17 dhidi ya Morocco, kisha itamalizana na Zambia na DR Congo katika hatua ya makundi.

Wiki hii, Kiseto ameingia kwenye orodha ya washindi kwenye droo ndogo inayotoa zawadi ya runinga ya nchi 70, dishi na dekoda yenye kifurushi kila wiki kwa washindi wawili na pesa taslimu kila siku.

Akizungumza wakati wa kukabidhi zawadi kwa mshindi wa wiki hii, mwakilishi wa Tigo Dar es Salaam, Justine Lawena, alisema bado fursa za kushinda pesa taslimu kila siku na runinga nyingine kila wiki ipo.

„Unapoendelea kubashiri na Betika kupitia akaunti ya Tigopesa ndipo unajiweka kwenye nafasi kubwa ya kushinda zawadi mbalimbali na kuingia kwenye droo ya Twende zetu Ivory Coast Ki-VIP," alisema.

Kwa upande wake, Kiseto alisema ataendelea kucheza hadi Januari 2 kwenye droo kubwa kwenda Ivory Coast kushuhudia AFCON.

„Nitaendelea kucheza zaidi na zaidi hadi kwenye droo kubwa kwani lengo langu ni kwenda Ivory Coast," alisema.

Mwakilishi wa Betika, Clinton Charles, alisema ni rahisi kupata nafasi ya kwenda Ivory Coast kushuhudia mubashara Afcon.

„Unachotakiwa ni kuweka pesa kwenye Tigopesa yako na kubeti na Betika," alisema na kuongeza.

„Pia zawadi nyingine za kila siku na kila wiki za pesa taslimu na runinga, inaendelea hadi Januari 2 itakapofanyika droo ya washindi sita watakaokwenda Ivory Coast kwenye Afcon.

Wiki ya kwanza washindi wawili kutoka Dodoma walishinda zawadi za wiki, wiki ya pili washindi kutoka Tanga na Lindi pia walikabidhiwa zawadi zao.

Michezo
Ijumaa Desemba 29, 2023
Nipashe

Haaland kurejea Januari mwishoni UKURASA 21





Mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Tanzania Bara, Kilimanjaro Stars', Kibu Denis (kushoto), akiwania mpira na mchezaji wa Timu ya Taifa ya Zanzibar, Zanzibar Heroes' wakati wa mchezo wa kirafiki jana uliochezwa Uwanja wa Amaan Zanzibar. Timu hizo hazikufungana. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA SC YASAJILI WINGA MCOLOMBIA

## ●●● Winga huyo kutua nchini wiki ijayo kukamilisha usajili huo huku Kocha Benchikha akitaka...

**Na Adam Fungamwango**

KAMA mambo yataenda yalivyopangwa, Jumanne ijayo Simba inatarajiwa kumpokea winga Mauricio Cortes Nunez mwenye umri wa miaka 26 raia wa Colombia kwa ajili ya kukamilisha taratibu za mwisho za usajili, huku klabu hiyo ikikiri kuwa inafanya usajili wa nguvu ambao itautangaza baadaye.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, amewatoa hofu wanachama na mashabiki wa klabu hiyo juu ya usajili kwenye dirisha hili dogo.

„Watu wanaendelea kusajiliwa huko nyuma ya pazia, ni usajili wenye tija kwa klabu yetu, mashabiki na wanachama watulie mambo yatakapokamilika tutawatangazia kila kitu," alisema Ahmed.

Ingawa hakutaja majina ya wachezaji ambao inawasajili, lakini taarifa za ndani ya klabu hiyo, zinasema tayari imempata winga huyo wa Colombia akitokea kwenye klabu ya Commerciantes huku ikielezwa kuwa atapewa mkataba wa miaka miwili.

Wachezaji wengine wanaohusishwa kujiunga na timu hiyo ni beki wa kushoto Hernest Briyock Malonga anayeichezea klabu ya CSMD Diables Noirs ya Congo Brazaville, kiungo mshambuliaji Miche Mika wa FC Saint Eloi Lupopo wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, na kiungo mkabaji Erick Mbangossoum raia wa Chad anayeichezea klabu ya Union Touarga ya nchini Morocco.

Kwa upande wa wachezaji wa Kitanzania, taarifa zinasema klabu hiyo tayari imekamilisha usajili wa Ladack Chasambi kutoka Mtibwa Sugar anayecheza nafasi ya winga na kiungo mshambuliaji, ambapo Ofisa Habari wa timu hiyo, Thobias Kifaru amesema wameshamalizana naye na kumruhusu kwa baraka zote, huku pia Wekundu wa Msimbazi wakiwa kwenye mazungumzo na wachezaji wengine, Edwin Barua wa Prisons anayecheza nafasi ya pembeni na mshambuliaji, Valentino Mashaka wa Geita Gold.

# Yanga kupeleka 'full nondo' Zanzibar, yamkana Sankara

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Yanga imesema itapeleka kikosi chake chote mjini Zanzibar kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi iliyoanza jana huku pia ikikanusha taarifa zilizoenea kuwa itakwenda na kikosi cha pili.

Pia uongozi wa klabu hiyo umeweka wazi haina mpango wa kumsajili mshambuliaji Sankara Karamoko kutoka Asec Mimosas kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe amesema jana kuwa, Kocha Mkuu, Miguel Gamondi amewaambia wachezaji wake wote kuwa yeyote ambaye hajachaguliwa kwenye kikosi cha timu ya taifa na si majeruhi, basi ana wajibu wa kuambatana na kikosi hicho mjini Zanzibar.

„Tunapeleka kikosi chetu chote Zanzibar, isipokuwa wale ambao wameitwa kwenye kikosi cha timu ya taifa na wale majeruhi tu, wote waliokuwa fiti watakwenda kucheza Kombe la Mapinduzi, kocha Gamondi amewaambia wachezaji kuwa hatokubali udhuru wowote wa mchezaji ambao utamkosesha kwenda huko," alisema Kamwe.

Kauli hiyo imekuja baada ya kuwepo kwa tetesi kuwa Yanga ingepeleka kikosi cha wachezaji ambao hawapati nafasi kwenye kikosi cha kwanza huku mastaa wake wakitajwa kwenda mapumziko mafupi baada ya ligi kusimama.

„Lazima twende kamili ili tukawape furaha mashabiki wa Yanga Zanzibar, kwa hiyo nawaambia wote watakuwepo hadi Skudu (Mahlatse Makudubela) atakuwepo.

Yanga itaanza mechi ya kwanza ya michuano hiyo Jumapili, itakapocheza dhidi ya Jamhuri.

Kamwe alisisitiza kuwa siku hiyo klabu itamtambulisha mchezaji mpya kama ambavyo wameshatangaza awali.

„Hatujabadilisha, siku hiyo pia kuna sapraizi, tunatarajia kutambulisha mchezaji wetu mpya kama ambavyo tumeshasema na tunarudia ni mchezaji ambaye wengi wanamfahamu," alisema Kamwe.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >